DIAGEO



# *Kanuni* Zetu

# Sote tunaweza kufanya jambo sahihi, kila wakati

Tumeaminiwa kufanya maamuzi sahihi kwa kutumia akili ya kawaida na maamuzi huku tukifanya kazi kulingana na maadili na malengo ya Diageo.

Kama hutapata mwongozo unaotafuta kwenye Kanuni zetu, sera au viwango, unapaswa kujiuliza:

**Je, matendo yangu yanaenda sambamba na malengo na maadili ya Diageo?**

Je, kipo kisheria?

Ndiyo →

Je, kinaendana na maadili ya Diageo na Kanuni zetu?

Ndiyo →

Je, kinaonekana kuwa sahihi?

Ndiyo →

Je, nitafurahia kueleza kile nilichofanya kwa wafanyakazi wenzangu, marafiki na familia?

Hapana/Sina uhakika ↓

## Acha! Tafuta ushauri na mwongozo

Kama jibu la maswali haya ni 'hapana' au 'sina uhakika' basi usiendelee.

**Daima, ni vizuri kuuliza swali kuliko kubahatisha jibu.**

Mwongozo wa nani wa kuongea naye ili upate msaada ama ushauri, na jinsi ya kutoa malalamiko, unaweza kupatikana katika ukurasa wa 45 (sehemu ya ndani ya jalada la nyuma).

# Lengo letu

*Kusherehekea maisha,* **kila siku, mahali popote**

## Maadili Yetu

- Tunawajali sana wateja wetu na watumiaji bidhaa zetu
- Kuwa bora zaidi
- Uhuru wa mafanikio
- Tunajivunia kile tunachofanya
- Kuthaminiana

## Kanuni Zetu

- Tunajali biashara yetu na tunahakikisha tunafikia viwango vya juu kabisa vya maadili ya kibiashara na tabia
- Tunatarajiwa kuonyesha uadilifu binafsi, na kuishi kwa kuzingatia maadili na tabia zinazoimarisha kazi zetu zote, kila siku, mahali popote

# Wapendwa wafanyakazi wenzangu,

**Lengo letu ni kuwa mojawapo ya kampuni bora, yenye bidhaa zinazoaminika na kuheshimiwa ulimwenguni.**



Hii inatuhitaji pia kuwa biashara inayosimamiwa vyema katika kategoria yetu, tukiweka viwango ili wengine wafuate.

Ili kujenga imani na heshima kwa kila mtu ambaye tunakutana naye kwenye kampuni yetu, ni muhimu kwamba tuongeze kiwango cha kile tunarejelea kama kuwa biashara yenye maadili na kuwa bora zaidi popote tunapoishi, kazini, tunaponunua na tunapouza. Kufanya biashara kwa njia ifaayo, kutoka mwanzo hadi mwisho, huhakikisha kuwa tunaafiki matarajio ya nje na viwango vyetu na kuwezesha biashara yetu kukua kwa njia endelevu na kwa kuwajibika.

Kanuni ya Maadili ya Biashara ya Diageo imeundwa ili kukusaidia kuelewa wajibu wako kama balozi muhimu wa biashara yetu na mtunzaji wa chapa na sifa zetu. Kanuni zetu hutoa maelezo kuhusu maeneo muhimu ya shughuli zetu za biashara na inaelezea majukumu ambayo sote tunayo kama wafanyikazi.

## Tunachotarajia kutoka kwako

Ni jukumu la kila mmoja wetu kulinda sifa zetu na kufanya kazi kwa uadilifu wa hali ya juu. Bila kujali majukumu, cheo au mahali ulipo, unapaswa kufuata Kanuni zetu, sera pamoja na sheria zote zinazohusika, taratibu na viwango vya kitasnia vinavyohusiana na kazi yako, wakati wote.

Tafadhali soma Kanuni na, kwa usaidizi kutoka kwa msimamizi wako, hakikisha unaelewa maana ya hii kwa kazi yako na unajua ni nani wa kumwendea ili kupata kusaidiwa.

Kanuni hii haitashughulikia kila hali unayokabiliana nayo, haswa katika ulimwengu huu unaobadilika na unaoshika kasi. Ingawa Kanuni zetu ni mfumo wa kutusaidia kupitia maamuzi ya kila siku, ni muhimu vile vile kutumia akili timamu na uamuzi mzuri, na kutenda kwa njia zinazounga mkono maadili na madhumuni yetu pekee. Kila tunachofanya na kusema ni onyesho la umahiri na tabia zetu, kwa hivyo ikiwa una shaka au una wasiwasi wowote, omba kuelekezwa na usiogope kuongea.

**Asante kwa kutekeleza sehemu yako na kuhakikisha kwamba biashara yetu iko katika hali bora zaidi leo na kwa vizazi vijavyo.**



Debra Crew
Mtendaji Mkuu



# Yaliyomo


Mwongozo wa Kanuni Zetu ....04
Majukumu Yetu ....05

**Maadili yetu binafsi** .... 06

Watu wanaamini kuwa tutatenda kwa kuzingatia maslahi ya Diageo na jamii

Kunywa kwa uangalifu ....08
Biashara kwa kutumia taarifa za ndani .... 09
Mgongano wa maslahi .... 10

**Maadili yetu ya kibiashara** ....12

Walinzi wa heshima ya Diageo

Masoko na ubunifu ....14
Zawadi na burudani ....15
Rushwa na ufisadi ....16
Serikali na vyama vya kisiasa ....17
Biashara haramu ....19
Ushindani ....20
Ulaghai ....21
Utakatishaji fedha na kusaidia ukwepaji kodi ....22
Vikwazo ....23

**Watu wetu** ....24

Kuthaminiana na kuheshimu watu wengine:

Afya, ulinzi na usalama binafsi ....26
Ubaguzi na unyanyasaji ....27
Haki za binadamu ....28

**Mali Zetu na taarifa** ....29

Kuwa kama wamiliki

Usimamizi wa taarifa na usalama ....30
Usiri wa data na taarifa binafsi ....32
Mali na rasilimali za kampuni ....33
Rekodi za biashara ....34

**Jamii na washirika wetu** ....35

Tunajivunia na mahusiano tunayoyaendeleza

Ubora ....36
Uendelevu wa Mwanzo hadi Mwisho ....37
Michango ya hisani ....38
Mawasiliano ya nje na mitandao ya kijamii ....40
Mahusiano na wateja, wasambazaji bidhaa na washirika wengine wa biashara ....42

**Unachohitaji kusoma** ....43
Msaada, ushauri na kutoa malalamiko ....45

# Mwongozo wa Kanuni Zetu

Kanuni zetu zinakusudiwa kuimarisha malengo na maadili yetu, na zina mwongozo wa majukumu yetu ya pamoja na ya binafsi ili kufanya biashara kwa mujibu wa majukumu hayo, na kufuata sheria zote zinazohusika, masharti na viwango vya kitasnia.

**Malengo yetu *na maadili***

**Malengo na maadili yetu** yanajenga msingi wa biashara yetu: yanatufanya sisi kuwa tulivyo na kuimarisha mafanikio yetu.

**Kanuni Zetu**

**Kanuni Zetu** hutoa taarifa kuhusu **nyanja muhimu za shughuli zetu za biashara** na inabainisha majukumu yetu sote kama wafanyakazi. Katika sehemu zinazofuata utapata mwongozo kuhusu **kanuni kuu** ambazo zinafaa kudhibiti jinsi unavyotenda.

Sera Zetu za *Kimataifa*

Sera zetu za Kimataifa zinaunga mkono Kanuni zetu na hutoa maelezo zaidi pamoja na mwongozo. **Lazima uzingatie Sera yoyote ya Ulimwenguni** inayohusu jukumu lako, bila kujali eneo lako. Sera Zetu za Kimataifa zinaweka kanuni ambazo tunatumia kimataifa kwenye shughuli zetu za biashara, zikijumuisha maeneo yote ambayo tuna wafanyakazi wetu.

Sera, *sheria na kanuni za ndani*

Pamoja na hayo kunaweza kuwa na **sera, sheria na kanuni** ambazo unahitaji kuzingatia, hivyo ni muhimu sana kujifahamisha shughuli yoyote muhimu.

Katika Mwaka wa Fedha wa 24, Diageo ilitangaza kuwa sarafu yake ya kuendesha shughuli za kazi imebadilika kutoka GBP hadi USD. Diageo pia imebadilisha sarafu yake ya uwasilishaji kuwa USD. Kwa hivyo, marejeleo yoyote ya takwimu za GBP yaliyo katika hati hii, yanapaswa kuzingatiwa kama USD. Ikiwa unahitaji ufafanuzi wowote, tafadhali wasiliana na mshiriki wa timu ya Uadilifu wa Biashara Kimataifa au Sanduku la Barua la Uadilifu wa Biashara **(Business.Integrity@diageo.com)**.

Kama huwezi kupata unachohitaji katika Kanuni zetu, jaribu kutumia mwongozo wetu wa 'Fanya jambo sahihi' uliopo katika jalada la mbele. Pia utapata mapendekezo kuhusu wapi pa kupata msaada, ushauri na jinsi ya kutoa malalamiko ndani ya jalada la nyuma.



# Wajibu wetu

## Kila mfanyakazi anapaswa kuwa mlinzi wa maadili na sifa yetu

**Jukumu la kulinda sifa ya kampuni kuifanya iwe kampuni inayoaminiwa na iwe mahala pazuri pa kazi ni letu sote.**

Unatarajiwa kuonyesha uadilifu binafsi, kuishi kwa maadili na kuonyesha tabia ambazo zinaimarisha kazi zetu zote. Hususan, kila mfanyakazi anatakiwa kuzingatia Kanuni zetu, sera zetu na sheria zinazohusika, miongozo na viwango vya kitasnia. Kushindwa kufanya hivyo kunaweza kusababisha kuharibu sifa na hasara ya kifedha kwa Diageo, na kunaweza kusababisha hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi yako, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi, na pia uwezekano wa kushtakiwa kwa kosa la jinai.

## Majukumu ya wasimamizi

Kanuni zetu na sera zinatumika kwa kila mtu, bila kujali nafasi zao au cheo - lakini wasimamizi wanatarajiwa pia kuwa mfano wa kuigwa. Kama unasimamia watu, unapaswa kuhakikisha kwamba watu wote kwenye timu yako wanapokea mwongozo, rasilimali na mafunzo wanayohitaji ili kuelewa kile kinachotarajiwa kutoka kwao.

**Unapaswa:**

- Uishi kwa mujibu wa maadili yetu na utetee kilicho cha haki
- Ujue Kanuni na sera zetu, na uhakikishe timu yako inafanya hivyo pia
- Uifundishe timu yako kufanya jambo linalofaa na kusifia tabia njema
- Uhimize kutoa malalamiko, kuyasikiliza na kuwasaidia wafanyakazi wanaofanya hivyo
- Uhakikishe hakuna kulipiza kisasi kwa anayetoa malalamiko

## Washirika wa kibiashara wa nje

Tunataka kufanya biashara na washirika ambao wanafuatilia maadili yetu. Tunahimiza washirika wetu wote kufuata maadili ya biashara kama vile kwenye Kanuni zetu, na mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya Diageo ni lazima ahakikishe kwamba matendo yake yanazingatia Kanuni na sera zetu.

Iwapo unawajibika na mahusiano na mshirika wa kibiashara, unapaswa kuhakikisha shughuli zao zinaafikiana na viwango vyetu. Ili kupata mwongozo, tazama ukurasa wa 42.




# Maadili yetu *binafsi*

*Watu wanaamini kuwa* tutatenda kwa kuzingatia maslahi ya Diageo na jamii

Kunywa kwa uangalifu

Biashara kwa kutumia taarifa za ndani

Mgongano wa maslahi

# Kunywa kwa uwajibikaji

## Sisi ni mabalozi wa unywaji pombe kwa uangalifu

Tunajivunia tunayofanya na tunaendeleza utamaduni - ndani na nje ya Diageo - ambapo watu wazima ambao wanachagua kunywa pombe, wanakunywa kwa uangalifu. Sote tunapaswa kuwa mabalozi kulinda sifa ya Diageo na kuendelea kuhamasisha unywaji pombe kwa kiasi.

Tunauza bidhaa zetu kwa uangalifu na tunafanya kazi kwa kushirikiana na serikali, jamii, watu binafsi, asasi zisizo za kiserikali na makampuni mengine ili kukabiliana na matumizi mabaya ya pombe ikiwa ni pamoja na unywaji pombe kupindukia, kunywa na kuendesha gari, na unywaji pombe kwa watoto.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- kufurahia pombe **kama sehemu ya maisha yenye msawazisho** (ukiamua kuitumia)
- **kutoruhusu** utendaji na uamuzi wako kazini uathiriwe na pombe kamwe
- **kuheshimu** umri halali wa kunywa pombe katika masoko yote na kutii sheria zinazohusiana na vileo
- **kupata ushauri wa matibabu au ushauri nasaha** kwa ajili yako mwenyewe ikiwa unapambana na tatizo linalohusiana na pombe
- **kuripoti** kosa lolote linalohusiana na pombe na/au kukamatwa kwa msimamizi wako.

DRINKiQ.com

Malengo yetu ni kusherehekea maisha ya kila siku, kila mahali na tunahamasisha wafanyakazi wetu na watumiaji kusherehekea kwa uangalifu. Kupitia DRINKiQ tunatoa ufahamu kuhusu unywaji pombe kwa makini na kusaidia kufanya maamuzi bora kuhusu kunywa au kutokunywa pombe. Tunaitangaza DRINKiQ.com katika chapa zote za Diageo, na kila mfanyakazi wetu lazima apitie mafunzo ya DRINKiQ.

# Maswali na Majibu

**Jana, mmoja wa wanatimu yangu alikuja kazini akiwa ananuka pombe na hakuwa tayari kwa mkutano muhimu. Ilibidi aondoke kwenye mkutano kwa sababu alikuwa mgonjwa na nikalazimika kumwakilisha. Hii si mara yake ya kwanza kufanya hivyo na hali hii inaathiri utendaji wake. Ninapaswa kufanya nini?**

Hakuna mtu anapaswa kuruhusu matumizi ya pombe kuathiri utendaji wake wa kazi, kwa sababu inaweza kusababisha matokeo mabaya kwa mfanyakazi au kwa kampuni. Kwanza, pendekeza atafute ushauri kutoka timu ya taaluma ya afya ikwa anahisi kuwa na tatizo la unywaji pombe. Pili, unapaswa kuzungumza na idara ya Rasilimali watu kwa ajili ya mwongozo na usaidizi ili kujua namna bora ya kusimamia utendaji wake.

**Nilikuwa narudi nyumbani nikiendesha gari baada ya kusherehekea siku ya kuzaliwa ya rafiki yangu. Polisi walinisamamisha na wakakuta nimepitiliza kiwango cha kunywa pombe wakati naendesha gari. Sikumjeruhi mtu yeyote, ilikuwa nje ya muda wa kazi na sikuwa nakwenda kazini. Kuna haja ya kuripoti jambo hili?**

Tunatambua kwamba jambo hili lilitokea katika muda wako binafsi, hata hivyo, ni lazima utoe taarifa kwa msimamizi wako kwa sababu wafanyakazi wote wana wajibu wa kusimamia maadili ya Diageo kuhusu unywaji pombe kistaarabu. Tovuti ya DRINKiQ ina taarifa ya kukusaidia kufanya maamuzi sahihi kuhusu kunywa au kutokunywa.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43

# Biashara ya taarifa za ndani

## Hatupaswi kufaidika kinyume cha sheria kutokana na taarifa tulizo nazo katika Diageo

Wengi wetu tunapata taarifa kuhusu hali ya kifedha au mipango ya baadaye ya kampuni za Diageo kupitia kazi zetu, baadhi ya taarifa hizo zinaweza kujumuisha 'taarifa za ndani'. Kutumia hii 'taarifa ya ndani' katika shughuli zako na hisa au dhamana ya Diageo au za kampuni nyingine za Diageo Group ambazo zimesajiliwa - 'taarifa za ndani' - ni kosa la jinai nchini Uingereza, Marekani, na nchi zingine nyingi. Ni wajibu wa kila mtu kuzingatia sheria zinazohusu taarifa za ndani za biashara.

Taarifa za ndani - au 'taarifa zisizo za umma' nchini Marekani - ni taarifa ambazo bado hazijachapishwa na, ikiwa zinapatikana, zinaweza kuwa na athari kubwa katika bei ya hisa au zinaweza kushawishi maamuzi ya wawekezaji kununua au kuuza hisa. Kununua au kuuza hisa, kuingia au kutoka katika mpango wa hisa, au kutoa hisa kama dhamana, zote hizi zinaweza kuwa za shughuli zinazopigwa marufuku kwa wale wenye taarifa za ndani. Sheria za taarifa za ndani kibiashara pia zinahusika kama utapanga mtu mwingine azitumie kuuza au kununua hisa - na zinaweza kutumika dhidi yako hata baada ya wewe kuondoka Diageo.

Ingawa utapewa ushauri na Katibu wa Kampuni iwapo Diageo itahisi kwamba unastahili 'kuwa na taarifa za ndani' wakati wa 'kufunga mwezi au mwaka', jukumu lako kuu litakuwa ni kuhakikisha hutoshiriki katika biashara inayohusisha taarifa za ndani.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kuwasiliana na** Sekretarieti ya Kampuni (utapata maelezo kwenye Mosaic) kabla ya kununua hisa za Diageo ikiwa una shaka.

# Maswali na Majibu

**Mimi ni msaidizi wa mtendaji mkuu, na nina uwezo wa kusoma taarifa nyingi za siri, ingawa sio tabia yangu kusoma habari hizo kwa kina. Ningependa kuuza baadhi ya hisa zangu za Diageo lakini mfanyakazi mwenzangu amependekeza kuwa inawezekana sitaweza kwa sababu ninafahamu 'taarifa za ndani'. Hii ni kweli?**

Ikiwa una taarifa ambazo watu wengine hawana na ambazo zinaweza kuathiri bei za hisa au kumshawishi mwekezaji, ina maana una taarifa za siri za ndani. Hata hivyo, sio taarifa zote za siri zaweza kuchukuliwa kama taarifa za ndani kwa minajili ya biashara ya hisa. Unapaswa kuuliza Sekretarieti ya Kampuni ikupe ushauri kabla ya kuuza hisa zako.

**Najua kwamba nina taarifa za ndani na hivyo wakati mwingine ninapata vikwazo kununua au kuuza hisa za Diageo. Hata hivyo, kaka yangu amenidokezea kwamba angependa kununua hisa za Diageo. Sijawahi kuzungumza naye kuhusu kazi yangu, kwa hivyo ni sawa?**

Unapaswa kuwa mwangalifu katika hali hii na kuwa na uhakika kwamba hakuna taarifa ambazo umemweleza ndugu yako ambazo zinaweza kuchukuliwa kama taarifa za ndani. Unapaswa kumwambia ndugu yako asinunue hisa hadi hapo utakapojadiliana na Katibu wa Kampuni, ambaye atakushauri kuhusu mambo yanayokubalika na yasiyokubalika.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43

# Migongano ya maslahi

## Sote tuna wajibu wa kutenda jambo kwa maslahi ya Diageo wakati wote

Migongano ya maslahi inaweza kutokea kama unaweka mbele maslahi yako binafsi, ya familia, fedha, kisiasa au maslahi mengine yanayoingiliana au kuwa na mvutano na uaminifu wetu kwa kampuni au uwezo wetu wa kufanya maamuzi sahihi kwa maslahi ya Diageo. Diageo inatarajia wafanyakazi wote kusema kwa ukamilifu migongano ya maslahi na kampuni kwa haraka mara tu baada ya kutambua tatizo hilo ili tuweze kuchukua hatua zinazotakiwa. Katika kesi nyingi, inatosha tu kuongea na msimamizi wako kuhusu migogoro ili kutatua tatizo; katika hali ngumu zaidi, hatua zingine zinaweza kuhitajika.

### Fanya jambo sahihi

Ili kuhakikisha kwamba maafikiano yako na Diageo hayawezi kuathirika, iwapo kuna uwezekano wa kuwa na mgongano wa maslahi, unapaswa:

- **kufichua** mgongano wowote wa maslahi unaoweza kutokea haraka kulingana na mchakato uliokubaliwa
- **kuhifadhi kumbukumbu** ya ufichuzi wowote na hatua zilizokubaliwa
- **kuwa macho** ili utambue hali zozote mpya zinazoweza kutokea za mgongano wa maslahi au mabadiliko ya ufichuzi uliopo unaoweza kutokea wakati wa ajira yako katika Diageo na ufichue mambo haya haraka na yanapotokea.

**Kama una wasiwasi jambo fulani linaweza kuwa la mgongano wa maslahi, haswa, ikiwa wewe ni Msimamizi wa Wafanyakazi na huna uhakika kama suala ulilofikishiwa linaweza kuwa na mgongano wa maslahi, tafadhali hakikisha kabla idhini yoyote haijatolewa na wasiliana na Msimamizi wa Maadili Kazini, mwanasheria wa kampuni au msimamizi wa Idara ya rasilimali watu ili kujadili suala hilo.**



## Maswali na Majibu

**Kuna nafasi ya kazi katika timu yangu ambayo nadhani mpwa wangu anaweza kuifanya. Nina wasiwasi wa kumpendekeza, kwa sababu ya uhusiano wetu. Je, nifanye nini?**

Ikiwa mpwa wako anatimiza masharti ya nafasi hiyo na ataleta natija kwa idara unapaswa kumwambia msimamizi wa ajira au msimamizi husika wa rasilimali watu. Hata hivyo, hupaswi kujihusisha katika mchakato wa ajira hiyo na nafasi hiyo haipaswi kuwa mojawapo ya kazi unazosimamia moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

**Tumekuwa na urafiki mzuri na mteja – tunaonana mara kwa mara. Familia yangu imealikwa kwenye harusi ya binti yake. Ningependa kuhudhuria harusi na kupeleka zawadi. Je, ni sawa? Nitanunua zawadi kwa pesa zangu.**

Mahusiano ya kazi na ya binafsi mara nyingi huingiliana. Jambo muhimu ni kwamba uhakikishe hakuna mtizamo wa mgongano wa maslahi kati ya mahusiano hayo. Unapaswa kuwa wazi kwamba utahudhuria harusi hiyo na kutoa zawadi uliyonunua kwa gharama yako mwenyewe, na si kama mwakilishi wa Diageo. Pia ni lazima umweleze msimamizi wako na uandike mahali.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43







### Je, mgongano wa maslahi ni nini?

Mgongano wa maslahi unaweza kutokea kutokana na hali mbalimbali. Mifano ya mgongano wa maslahi ni pamoja na:

- kushiriki katika shughuli ambazo zinaweza kushindana na Diageo – kwa mfano, kushiriki katika biashara nyingine au kuwa na kazi isiyo ya Diageo ambayo inaathiri uwezo wako wa kufanya kazi
- kuwa na maslahi ya kifedha au cheo unakolipwa katika kampuni ambayo inafanya biashara na Diageo moja kwa moja au kwa namna nyingine ambayo Diageo ina maslahi ndani yake
- kuruhusu maamuzi yako ya kazi yawe, au kuonekana kuwa, yanasukumwa na maslahi ya kibinafsi au ya kifamilia au ya kirafiki – ikiwa ni pamoja na kukodisha au kumsimamia ndugu au mtu ambaye mna uhusiano wa karibu
- kupokea fedha au mali yoyote kutoka kwa msambazaji bidhaa, mteja, au mshindani, au kampuni ambayo inafanya biashara na Diageo
- kutumia mali ya kampuni, taarifa au rasilimali kwa manufaa yako binafsi au kwa faida ya wengine kwa njia ambayo hairuhusiwi na Diageo.

### Je, ninaweza kuwa katika hali ya mgongano wa maslahi?

Kama ukijibu 'ndiyo' kwa mojawapo ya maswali haya lazima utoe taarifa juu ya mgongano wa maslahi unaoweza kutokea kwa msimamizi wako.

- je, uhusiano wangu na mteja wa Diageo, msambazaji bidhaa, kampuni yenye ushirika au mshindani unaweza kutiliwa shaka?
- je, hali hii inaweza kudhoofisha uwezo wangu wa kufanya maamuzi ya kibiashara kwa maslahi ya Diageo?
- je, ni mimi, au ni mtu wangu wa karibu, anayeweza kufaidika na ushiriki wangu katika suala hili?
- je, kuna uwezekano kwamba maamuzi yangu yanaweza kuleta wasiwasi au kuonekana kama hayawezi kuwa na maslahi ya Diageo?
- je, ushiriki wangu katika shughuli hii unaathiri uwezo wangu wa kufanya kazi?




# Maadili yetu *ya kibiashara*

## Walinzi wa heshima ya Diageo

Masoko na ubunifu

Zawadi na burudani

Rushwa na ufisadi

Serikali na vyama vya kisiasa

Biashara haramu

Ushindani

Ulaghai

Utakatishaji fedha na kusaidia ukwepaji kodi

Vikwazo

# Kutafuta masoko na ubunifu

### Lazima tuhakikishe kwamba bidhaa zetu zinatangazwa na kuuzwa kwa makini

Tunataka shughuli za masoko na utangazaji za Diageo zitambulike kama bora ulimwenguni, na tunajivunia ya kwamba bidhaa zetu zinaleta burudani kwa mamilioni ya watu kila siku. Hata hivyo, tunatambua kwamba pombe inaweza kunywewa bila kipimo, na kuleta matatizo kwa watu binafsi na jamii.

Kanuni za Biashara za Diageo (DMC) na Kanuni ya Kidijitali ya Diageo (na Miongozo yake ya Ufichuaji iliyoambatishwa ya Mshawishi na Muungaji Mkono na Miongozo ya Lazima ya Kimataifa ya Mitandao ya Kijamii) inatumika kwa shughuli zote za kutafuta masoko na/au shughuli za kutafuta masoko kidijitali na lazima ifuatwe, na kubainisha kwamba shughuli zetu zote za kutafuta masoko ni sharti:

- ziwalenge watu wazima pekee na sio vijana wenye umri mdogo wasioruhusiwa kisheria kununua pombe
- zionyeshe na kuhimiza unywaji pombe kistaarabu pekee
- zisiashirie kwamba chapa zetu za vinywaji vya pombe zinatoa faida zozote za afya, matibabu, lishe, au uwezo zaidi
- zisionyeshe au kuashiria kwamba unywaji pombe unaleta mafanikio ya kijamii au mengineo
- kijumla, zidhihirishe viwango vinavyokubalika vya nidhamu na adabu njema.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kufuata** DMC yaani Kanuni za Biashara za Diageo katika shughuli zote za masoko na utangazaji, zikiwemo za kidijitali
- **ufuate** mchakato uliopitishwa wa shughuli zote za masoko kama ilivyokubaliwa na kitengo cha biashara cha Diageo
- **uhakikishe** washirika wengine, kama vile kampuni za matangazo na za kidijitali zinazoshiriki katika shughuli za utafutaji wa masoko na matangazo kwa niaba ya Diageo wanafahamu na kutimiza masharti ya DMC
- **uhakikishe** kwamba rasilimali zote za masoko za kidijitali, ikiwa ni pamoja na rasilimali kwenye tovuti zilizohifadhiwa na washirika wengine, zinawekwa kwenye majukwaa ya Diageo yaliyoidhinishwa na idara ya Manunuzi kwa mujibu wa Kanuni ya Diageo ya Kijiditali na taratibu husika za usiri wa data ikiwa ni pamoja na, ikiwa inatumika, kanuni za GDPR).

# Maswali na Majibu

**Nimekuwa nikishiriki katika kampeni ya kutafuta masoko ya bidhaa mpya. Nina wasiwasi kwamba baadhi ya vigezo vya utangazaji vinaweza kuvutia vijana. Ninapaswa kufanya nini?**

Unapaswa umweleze msimamizi wako wasiwasi wako na utafute ushauri kutoka kwa mwidhinishaji wa DMC. Tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba matangazo yetu yanawalenga watu wazima pekee na hayajatayarishwa katika namna ya kuvutia vijana wenye umri mdogo wasioruhusiwa kunywa pombe kisheria.

**Nimepokea malalamiko kutoka kwa mfanyakazi mwenzangu aliyopo nchi nyingine ya kuwa mojawapo ya shughuli zetu za masoko hayaendani na DMC. Hatukupata malalamiko yoyote hapa na shughuli iliidhinishwa na waidhinishaji wote wa DMC. Je, napaswa kufanya chochote?**

Ndiyo, mwarifu msimamizi wako, mkurugenzi wa masoko wa nchi yako na mtaalam wa mambo ya DMC, ambao wanaweza kuamua kama masharti ya DMC yamekiukwa. Sheria na masharti ya maeneo tofauti yanaweza kutofautiana na sehemu nyingine huweza kuwa ni makali zaidi kuliko DMC.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43



# Zawadi na burudani

### Kamwe hatupaswi kutoa au kupokea zawadi au burudani ambazo hazifai

Kutoa na kupokea zawadi na burudani kunalenga kujenga uhusiano wa nje wa kibiashara na kukuza ushirikiano mwema. Hata hivyo, hatutakiwi kutoa au kupokea zawadi na burudani ambazo kufanya hivyo kunaweza kujenga hisia ya kuwajibika kutoa kitu kwa sababu hii inaweza kuonekana kama ni rushwa (angalia ukurasa wa 16).

### Fanya jambo sahihi

Kila unapotoa au kupokea zawadi na/au burudani, lazima ufuate Kanuni za Diageo za Zawadi na Burudani. **Mambo ya kuzingatia:**

- **kila wakati ni lazima upate kibali** cha mwanasheria wa ndani wa Diageo kabla ya kutoa, kumpa au kulipia zawadi yoyote au burudani kwa 'afisa wa serikali' (angalia ufafanuzi katika ukurasa wa 17)
- **usitoe** au kupokea fedha taslimu au zawadi zenye dhamana zinazolingana na fedha katika mazingira yoyote.
- **pata kibali cha msimamizi wako** kabla ya kutoa au kupokea zawadi kutoka kwa mtu wa nje:
  - zawadi zinazotoka au zinazopelekwa kwa kampuni fulani ambazo thamani katika mwaka wa fedha inazidi pauni £100* (au thamani ya pesa za eneo husika) kwa ujumla;
  - burudani ambayo hutokea mara kwa mara, inaweza isihusiane na kazi, au inaweza kuonekana kama ni kubwa sana au thamani yake ina mashaka
  - **kighairi:** Huhitaji kurekodi, au kupata idhini ya msimamizi wa kampuni ya, G&E ikiwa itapokelewa kutoka kwa maafisa wasio wa serikali na zawadi au burudani ni chini ya £100* (au sawa na sawa na sarafu ya nchi hiyo) kwa jumla. Kiasi hiki cha juu cha fedha ni sawa duniani kote, kwa matukio, na pia jumla ya jumla ya shirika katika bajeti fulani. Hii isiyofuata kanuni haitumiki kwa G&E iliyopokewa kutoka kwa maafisa wa serikali (kama neno hilo linavyofafanuliwa katika Sera yetu ya G&E) na HAKUNA kutumika kwa G&E inayotolewa kwa washirika wowote wa nje.
- **andika kumbukumbu vizuri na kikamilifu** ya zawadi zote na burudani ambazo umetoa, au ulizopokea kutoka kwa wahusika wa nje kwenye sajili yako ya zawadi na burudani
- **kamwe** usitoe au kukubali zawadi, burudani, au ukarimu kwenda/kutoka kwa wakaguzi wa nje wa kampuni nyingine isipokuwa tu kama inakubalika.

**Au thamani ya chini ikiwa imebainishwa kwenye sera ya mahali husika.*

### Je, udhamini na motisha za kibiashara ni sawa na zawadi?

Hapana. Wakati tunapotoa zawadi, huwa hatutarajii kupata kitu chochote. Sisi tunatoa motisha za kibiashara au kudhamini watu wengine ili tupate faida ya kibiashara iliyokubaliwa.

Idhini ya awali ya mwanasheria wa ndani wa Diageo inahitajika kwa udhamini na motisha za biashara iwapo inamhusu afisa wa serikali.

Tazama mwongozo kuhusu Zawadi, Burudani na Udhamini kwa Maafisa wa Serikali kwenye fomu ya Maombi ya Idhini ya Awali kwenye Mosaic.

### Zawadi inayolingana na pesa taslimu ni nini?

Kadi ya zawadi, cheti au vocha huzingatiwa kama zawadi sawa na pesa taslimu na haiwezi kukubaliwa kutoka kwa mshirika yeyote wa kibiashara, bila kujali thamani yake. Sera yetu inakataza kutoa au kukubali zawadi za pesa taslimu au zawadi zinazolingana na pesa taslimu.

# Maswali na Majibu

**Nimepokea kikapu cha chakula kutoka kwa mteja, yenye thamani ya pauni £50. Mteja huyo huyo alinitumia chupa mbili za mvinyo mapema mwaka huu, kila chupa ina thamani ya pauni £40. Ninajua thamani ya jumla inapita pauni £100* lakini sikuweza kupata idhini ya Msimamizi wangu wa Wafanyakazi kabla ya kupokea kikapu hicho cha chakula kwa kuwa sikujua kama ningeipokea. Ninapaswa kufanya nini?**

Unapaswa kuwasiliana na Msimamizi wako wa Wafanyakazi mara moja na mwambie kila kitu ulichotumiwa na mteja huyu katika mwaka huu wa fedha. Ikiwa atakubali kwamba unaweza kukubali, hakikisha anathibitisha kwa maandishi, mshukuru mteja wako kwa zawadi na iorodheshe kwa usahihi kwenye sajili ya zawadi na burudani yani (G&E). Ikiwa Msimamizi wako kakukatalia, basi utapaswa kurudisha zawadi hiyo. Ikiwa haiwezekani kurudisha (mfano, kwa sababu ni bidhaa inayoharibika au inaweza kusababisha mahusiano kuharibika), basi inapaswa kutolewa kwa timu yako au kutolewa kama zawadi kwa njia ya bahati nasibu. Hii pia inapaswa kurekodiwa kwenye kumbukumbu za taarifa za zawadi na burudani (sajili ya G&E).

**Ninaandaa tukio la biashara kuitangaza Baileys. Kila mhudhuriaji atapokea chupa ya mililita 50 kwa ajili ya kuonja. Je, ninapaswa kurekodi kutoa sampuli hizi kama zawadi kwenye sajili yangu ya zawadi na burudani?**

Chupa ya sampuli ya bidhaa ya Diageo, inapotumika kwa makusudi ya kuitangaza pekee, haichukuliwi kama zawadi. Kwa hiyo haipaswi kurekodiwa kwenye rejista yako ya zawadi na burudani. Hata hivyo unapaswa kuhakikisha chupa zote za sampuli zimehesabiwa kwa ajili ya matumizi ya uanzishaji na kukuza masoko ili kujua utendaji wa bidhaa zisizolipiwa.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43

# Rushwa na ufisadi

### Haturuhusu rushwa au ufisadi wa namna yoyote ile

Sisi tunajivunia sifa yetu kama kampuni inayoaminika na kuheshimiwa. Hatuwezi kuruhusu aina yoyote ya ufisadi, moja kwa moja au kwa namna nyingine, kufanywa na wafanyakazi au wawakilishi wetu. Hatutoi, kumpa, au kupokea, rushwa au faida nyingine isiyofaa kwa maslahi ya kibiashara. Sheria hiyo inatumika kwa aina yoyote ya rushwa ya thamani yoyote, na haitumiki tu kwa fedha.

Ni lazima wote tuwe waangalifu sana na kuhakikisha kwamba vitendo vyetu havitafsiriwi kuwa rushwa, hasa katika mambo ya zawadi, ukarimu, burudani, matumizi, usafiri, motisha za biashara, michango ya kisiasa, michango kwa mashirika ya kujitolea, ushawishi, na udhamini. Pia hatuna budi ya kuhakikisha uhusiano wetu na washirika wetu wa kibiashara na kuhakikisha maafisa wa serikali hawaleti mazingira ya hongo au ufisadi itakayohatarisha Diageo.

Ni muhimu kuweka kumbukumbu za miamala yote kikamilifu na kwa usahihi katika rekodi zetu za uhasibu na fedha.

Kama umeombwa upokee au utoe rushwa lazima ukatae - na lazima utoe taarifa hiyo mara moja kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo au toa taarifa kupitia huduma ya SpeakUp.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **usithubutu** kutoa, kuidhinisha, au kupokea rushwa, ikiwa ni pamoja na 'malipo ya kurahisisha' (yaani malipo madogo ili kuharakisha kile kinachotakiwa kuwa utaratibu wa serikali), au aina yoyote ya malipo haramu kwa nia ya kupata manufaa au faida ya kibiashara kwa Diageo
- **kufuata kila mara** Sera ya Kimataifa ya Zawadi na Burudani na Sera yetu ya Kimataifa ya Kupambana na Ufisadi **kuhakikisha** kwamba taarifa zote za fedha ziko kamili na sahihi, na kwamba miamala ipo wazi na inaeleweka, na kwamba hakuna shughuli ya kibiashara isiyoeleweka, isiyorekodiwa, au isiyoelezeka vizuri
- **ongea na** mwanasheria wa ndani wa Diageo kuhusu masuala yoyote ya malipo ya pesa taslimu ya thamani yoyote kwa afisa wa serikali au mshirika yeyote wa biashara
- **usiombe** malipo yoyote kutoka kwa mshirika wetu wa biashara kwa maslahi yako binafsi
- **Fuata hatua zinazofaa katika mpango wetu wa** Mjue Mshirika wako wa Kibiashara (KYBP) kabla ya kuanzisha uhusiano na mshirika wa kibiashara kwa niaba ya Diageo na uhakikishe kwamba mshirika huyo hatahusika katika rushwa ama ufisadi.
- **rejelea sehemu za Kanuni yetu** zinazohusu misaada kwa Mashirika ya kujitolea (ukurasa wa 38), Serikali na vyama vya kisiasa (ukurasa wa 17) na Zawadi na burudani (ukurasa wa 15) kwa taarifa zaidi.

## Maswali na Majibu

**Niliambiwa nifanye malipo kidogo kwa mfanyakazi wa forodha ili bidhaa zetu zipitishwe haraka forodhani. Tunatakiwa kumpelekea mteja wetu bidhaa zake haraka iwezekanavyo na wala hatujavunja sheria za nchi. Ninapaswa kufanya nini?**

Diageo haipaswi kuwalipa maafisa ili watekeleze wajibu wao. Sheria ya Rushwa Uingereza inasema kwamba ni kinyume cha sheria kutoa malipo ya 'uwezeshaji' au 'kurahisisha' pale palipofanywa ombi - kwa hiyo ni marufuku kufanya malipo hayo, hata katika nchi ambazo malipo hayo si haramu. Ongea na msimamizi wako au mwanasheria wa ndani wa Diageo ili kuamua njia mbadala kwa mujibu wa sheria kutoa bidhaa zetu forodhani.

**Nimeambiwa kwamba njia bora ya kupata vibali ninavyohitaji kutoka serikalini ni kuajiri mshauri wa kufanya huduma hiyo. Nimekutana na mmoja na akaitisha mshahara shikilizi wa $50,000. Je, ninahitaji kuwa na wasiwasi kuhusu jinsi atakavyotumia hizo fedha kupata vibali?**

Ndiyo, una wajibu wa kuhakikisha kuwa uchunguzi wa kina unafanywa kabla ya kumhusisha mtu yeyote ambaye atakuwa anatangamana na maafisa wa serikali kwa niaba ya Diageo. Kabla ya mshauri kuajiriwa, wasiliana na mwanasheria wa ndani wa Diageo ili uchunguzi wa kina ufanywe na mipango sahihi ya mkataba ikamilishwe.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43**



# Serikali na vyama vya kisiasa

### Tunaweza kuzungumza na vyombo vya serikali au vyama vya kisiasa kama tuna kibali tu

Katika kufanya biashara, Diageo huwasiliana na maafisa wa serikali na wanachama wa vyama vya kisiasa duniani kote - lakini tunatakiwa kufanya hivyo kwa namna inayokubalika.

Hupaswi kushawishi au kufanya biashara kwa niaba ya Diageo na viongozi wa serikali, wabunge, wagombea wa kisiasa, wafanyakazi wengine wa serikali au mashirika ya umma bila idhini ya mkurugenzi wa mahusiano katika kampuni.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kuelewa** Sera ya Ushindani wa Kimataifa na Inayopinga Ushindani wa Kibiashara na sheria za ushindani zinazotumika katika soko lako
- **kutofanya** malipo au kugawa bidhaa au huduma, kama vile matumizi ya bure ya vitu vya Diageo kwa wanasiasa au vyama vya kisiasa, au kusaidia shughuli za kisiasa
- **kupata kibali mapema** kutoka kwa mwanasheria wa ndani kila wakati kabla ya kutoa, kugawa au kulipia zawadi yoyote, burudani au kumdhamini afisa wa serikali (angalia Zawadi na burudani kwenye ukurasa wa15)
- **kutoa** taarifa kuhusu mgongano wa maslahi kama una uhusiano na kikundi fulani cha kisiasa ambacho kazi yako inafanya uwasiliane nacho (angalia migongano ya maslahi katika ukurasa wa 10).

### Michango

Utamaduni wa Diageo si kutoa michango ya kisiasa, misaada au matumizi (isipokuwa tu katika mazingira machache sana, kukiwa na idhini ya kabla kutoka mkuu husika wa Mahusiano ya Kampuni na Shughuli za Kisheria).

Hauruhusiwi kutoa michango kama njia ya kushawishi serikali au chama cha siasa ili kutoa uamuzi kwa manufaa ya Diageo. Michango yoyote au huduma kwa vyombo vya siasa lazima uwe wazi na na itolewe kufuatana na sheria husika.

### Siasa zako binafsi

Diageo inatambua haki yako ya kushiriki kama mtu binafsi katika shughuli za kisiasa. Hata hivyo, ni lazima tuhakikishe kwamba shughuli hizo haziingiliani na kazi, na hairuhusiwi kutumia pesa au mali ya Diageo kwa ajili ya shughuli hizo. Hasa, Diageo inajitenga na shughuli zozote ambazo zinachochea siasa kali au kudhoofisha msimamo wetu wa kusherekea utamaduni mbalimbali na fursa sawa.

## Maswali na Majibu

**Mfanyabiashara ninayemfahamu amependekeza nikutane na rafiki yake ambaye ni mwanasiasa mashuhuri anayeweza kuisaidia Diageo katika biashara. Ninapaswa kufanya nini?**

Wasiliana mkurugenzi wa mahusiano ili upewe idhini - hupaswi kuwa na mawasiliano na mwanasiasa bila idhini hiyo. Kutegemea na mazingira wanaweza kukubaliana na wewe kwa baadhi ya vitu ili uweze kukutana na mwanasiasa huyo na kutoa taarifa utakapomaliza, au kukuarifu umtambulishe rafiki yako kwenye timu ya mahusiano ya kampuni, ambao watalishughulikia suala hilo.

**Nipo katika hafla na kuna mwanasiasa ameanza kuzungumza nami kuhusu biashara za Diageo. Ninapaswa kufanya nini?**

Kama ulijua mapema kwamba kwenye hafla hiyo kuna uwezekano wa wanasiasa kuhudhuria, ongea na mkurugenzi wa mahusiano kujiandaa namna ya kuongea na unayopaswa kusema. Iwapo mlikutana kibahati tu, jibu maswali kwa uaminifu lakini bila kufafanua taarifa yoyote ya siri, na, endapo inafaa, mtambulishe mwanasiasa huyo kwa timu ya mawasiliano ya kampuni.

**Chama tawala cha siasa katika eneo langu kinapanga sherehe zake za siku ya kuzaliwa na kimeomba timu ya Uhusiano wa Kampuni kuona kama Diageo inaweza kufadhili tukio hilo.**

Wasiliana na mwanasheria wa ndani wa Diageo ili kupata ushauri iwapo kufadhili tukio hilo kunaweza kuchukuliwa kama mchango wa kisiasa na ikiwa ndivyo, kama inawezekana kuendelea au la.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43**



**Afisa wa serikali ni nani kwa mujibu wa Kanuni Zetu?**

- maafisa na wafanyakazi wa matawi yote ya serikali, katika ngazi zote, ikiwa ni pamoja na jeshi na polisi
- maafisa na waajiriwa wa biashara zinazomilikiwa au kuendeshwa na serikali, ikiwa ni pamoja na mashirika ya misaada, na duka lolote la pombe linalofadhiliwa na serikali au vyombo vya habari vya serikali.
- maafisa na waajiriwa wa mashirika ya kimataifa ya umma (k.m. Umoja wa Mataifa), pia na wafanyakazi wa ubalozi
- watu binafsi wanaofanya kazi kama maafisa rasmi wa au kwa niaba ya yeyote alitajwa hapo juu.
- maafisa wa vyama vya kisiasa, wafanyakazi na wagombea nyadhifa za kisiasa
- ndugu ya familia ya kifalme
- watu binafsi ambao vinginevyo wamebainishwa kama 'maafisa wa serikali' chini ya sheria za mahali husika
- 'Watu Walio katika Mazingira ya Kisiasa' yaani,'maafisa wa serikali' waandamizi wa sasa na wa zamani, wanafamilia (yaani, wanandoa, wapenzi, watoto, na wanandoa wao au wapenzi, au wazazi) na washirika wa karibu wanaofahamika, ama kijamii au kitaalamu, na watu hawa binafsi.



# Biashara haramu

## Tunawajibika kulinda bidhaa zetu dhidi ya bidhaa bandia, na lazima tushiriki katika kutokomeza magendo

### Bidhaa bandia na zinazofanana

Tunapenda sana kuhakikisha kwamba wateja wetu wanakuwa na imani na bidhaa zetu na kuwa zina ladha nzuri na tamu. Bidhaa bandia na 'zinazofanana' zinaweza kusababisha wateja wasitambue kuwa ni bidhaa bandia, na kufikiria kuwa ni bidhaa halisi za Diageo, hivyo kuvunja imani nasi.

'Bidhaa zinazofanana' au 'zilizoigwa' hutumia majina yanayofanana, nembo, maumbo ya upakiaji, alama za biashara, muundo na rangi za bidhaa zetu halisi, mfano 'JOHNNY WALTER' badala ya 'JOHNNIE WALKER'. Bidhaa bandia zinalenga kufanana katika muonekano na bidhaa zetu halisi isipokuwa hazina ubora, na wakati mwingine zina sumu; mara nyingine chupa zetu hutumiwa na kujazwa bidhaa bandia.

Kama ukiona bidhaa unayofikiri kuwa ni ya bandia au imeigwa, unapaswa kutoa taarifa mara moja, ili Diageo iweze kuchukua hatua. Hii inaweza kufanywa kwa njia ya kutekeleza sheria ambayo inalinda haki miliki zetu, kama vile alama za biashara, hakimiliki, hatimiliki, siri za kibiashara, na majina ya bidhaa.

### Magendo

Bidhaa za magendo ni zile ambazo zinaingizwa nchini bila malipo au kodi inayotakiwa. Bidhaa zetu, sawa na za makampuni mengine ya vyakula na vinywaji wakati mwingine zinaingizwa kwa magendo katika masoko na watu wengine. **Hatutakiwi kusimamia, kuendeleza au vinginevyo kujihusisha na shughuli zozote za kimagendo.**

### Fanya jambo sahihi

- **unapaswa** kutoa taarifa ya bidhaa yoyote unayofikiri kuwa ni ya bandia, imeigwa au imeharibiwa kwa kupitia '**Spot and Stop**' kwenye Mosaic, au toa taarifa moja kwa moja kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo au wasiliana na afisa anayelinda ubora wa bidhaa
- **haupaswi kamwe** kusimamia, kuendeleza au kujihusisha kwa namna yoyote ile katika magendo. Ripoti malalamiko yoyote mara moja kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo.

# Maswali na Majibu

**Mmoja wa wateja wangu aliniambia kuwa amesikia kuna maduka fulani ya reja reja ambayo yananunua bidhaa zetu kutoka kwa maduka yasiyofahamika, na kwamba baadhi ya bidhaa hizo ni bandia. Ninapaswa kufanya nini?**

Omba upewe taarifa zote pamoja na maelezo yote haraka iwezekanavyo kutoka kwa mteja wako, ikiwa ni pamoja na maelezo ya bidhaa na maduka, na mwambie kwamba Diageo itashirikiana na mamlaka husika kufanya uchunguzi. Tuma taarifa zote ulizokusanya kwa afisa anayehakikisha bidhaa za kampuni na mwanasheria wa ndani wa Diageo, au kupitia '**Spot and Stop**' kwenye Mosaic.

**Hivi karibuni baadhi ya marafiki zangu walikuwa wanakunywa mojawapo ya pombe zetu katika baa na wote waliona kama haikuwa na ladha nzuri. Je, nitoe hii taarifa?**

Ndiyo, unapaswa kutoa taarifa ya suala hilo kupitia '**Spot and Stop**' au mjulishe afisa anayelinda ubora wa bidhaa za kampuni au mwanasheria wa ndani wa Diageo moja kwa moja ili waweze kuchunguza zaidi. Ukiukwaji wa bidhaa zetu unaweza kufanywa kwa njia nyingi na inawezekana bidhaa hizo zimebadilishwa au zinaweza kuwa ni za bandia.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43**

# Ushindani

**Ni lazima tutii sheria zote zinazokusudiwa kulinda na kukuza ushindani huru wa kibiashara na haki duniani kote**

Sote tunataka uhuru wa kufanikiwa - lakini mafanikio hayo lazima yawe yanafuata sheria na kuzingatia malengo na maadili yetu. Katika nchi nyingi, sheria za ushindani au ukiritimba husimamia ushirikiano na washindani, wateja, wasambazaji na wengineo. Sheria za ushindani hutumika pia katika nchi nyingine.

### Fanya jambo sahihi

**Unapaswa:**

- **kuelewa** sheria za ushindani zinazotumika katika nchi yako, na iwapo una wasiwasi wowote, tafuta ushauri kutoka kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo kuhusu mambo yanayokubalika.

**Kamwe hupaswi:**

- **kukubali au hata kujadili** na washindani: kupanga bei au masharti mengine ya kibiashara; kupunguza uzalishaji; kugawana maeneo au bidhaa au wateja; au kukataa kufanya biashara na mteja yeyote au msambazaji
- **kujadili** siri za kibiashara na washindani, kwa mfano bei, gharama, faida, masharti ya biashara, mipango ya masoko au uzinduzi wa bidhaa mpya
- **kutumia chama cha biashara** kama jukwaa la kujadili au kukubaliana kuhusu mbinu za kumvutia mteja au kujadili masuala ya kibiashara kama vile matangazo.

Kama ulikuwepo wakati suala kama hilo likiwa linajadiliwa, unapaswa kuondoka katika mkutano huo au kumaliza mazungumzo, na kumjulisha mara moja mwanasheria wa ndani wa Diageo.

### Muingiliano na washindani

Wakati unapokusanya habari za ushindani, daima fuata Miongozo ya Diageo kuhusu Ushindani.

Hairuhusiwi kutafuta au kukubali habari za siri za biashara kutoka kwa washindani.

Vile vile, usijaribu kutafuta au kukubali taarifa za siri za kibiashara kuhusu washindani kutoka kwa wateja au watu wengine.

Hata hivyo, iwapo wakati wa majadiliano ya bei, kwa kujitolea, mteja akalinganisha bei ya mshindani (kwa mfano 'Absolut ni $10 kwa kila boksi na ni nafuu zaidi kuliko Smirnoff'), unaweza kutumia na kuhifadhi taarifa hiyo.

### Muingiliano na wateja

Hairuhusiwi kujadili masharti ya mteja mmoja na mteja mwingine, na hairuhusiwi kuwatumia wateja kutuma taarifa za siri za kibiashara kwa washindani.

Katika nchi nyingi ni kinyume cha sheria kupanga bei, kupanga kiwango cha chini cha bei au kuwashawishi wateja wafuate bei zilizopendekezwa.

Nchi nyingi pia zinadhibiti wasambazaji kuweka vikwazo kama vile uwezo pekee wa kuuza bidhaa hiyo au kumdhibiti mteja kuuza tena bidhaa.

Hakikisha unajua sheria za nchi yako ili kuhakikisha huzivunji.



## Maswali na Majibu

**Mfanyakazi mwezangu alikuwa anafanya kazi kwa mshindani wetu. Alisema kwamba bado ana mkakati wa bei wa mwaka ujao kutoka kwa mwajiri wake wa zamani katika kompyuta mpakato yake, na aliniuliza iwapo ningependa kuiona. Ninapaswa kufanya nini?**

Mueleze kwamba huwezi kujadili au kupokea taarifa yoyote inayohusiana na bei za mshindani, na kwamba taarifa hiyo haipaswi kuonwa na mfanyakazi yeyote wa Diageo. Ikiwezekana, panga mkutane naye pamoja na msimamizi wako au na mwanasheria wa ndani wa Diageo ili kujadili hatua za kuchukua.

**Katika mkutano na mteja wa rejareja ili kujadili uzinduzi wa bidhaa mpya, alinionyesha faili kwenye kompyuta yake lililokuwa na maelezo ya kina kuhusu mipango ya matangazo ya kila mshindani kwa mwaka unaofuata. Ninapaswa kufanya nini?**

Mwambie mteja kwamba sio vizuri kwa wewe kupata taarifa za siri za kibiashara za mshindani, na umuombe afunge faili hilo. Piga ripoti kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo kuhusu suala hili mara moja, na usiandike maelezo yoyote kuhusu uliyoyaona au kumwambia mfanyakazi yeyote wa Diageo.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43



# Ulaghai

**Tumejitolea kuzuia, kupunguza, kugundua na kuchunguza shughuli zinazoweza kuwa za ulaghai.**

**Ulaghai ni kuwa mdanganyifu au kutumia njia zisizo za haki:**

(i) kujipatia faida wewe mwenyewe au kumfaidi mtu mwingine; au

(ii) kufanya mtu mwingine apate hasara. Tabia ya ulaghai imepigwa marufuku kabisa katika Kampuni ya Diageo.

**Mtu yeyote anaweza kuwa mwathiriwa au mhalifu wa ulaghai. Kampuni ya Diageo inaweza kudanganywa na wafanyakazi wake au wahusika wengine; vivyo hivyo, wahusika wengine wanaweza kudanganywa na wafanyakazi wa Diageo.**

### Fanya jambo sahihi

- Usiwahi kujihusisha katika shughuli yoyote kwa kimakusudi, isiyohusu uaminifu, inayohusisha mali au taarifa za fedha na uhasibu wa Diageo au wahusika wengine.
- **Unahitaji kufahamu na kufuata** Kanuni, Sera, Miongozo, Taratibu na Viwango vya Kompyuta ya Mezani vya Diageo
- Unatarajiwa **kuripoti shughuli** yoyote inayoshukiwa kuwa ya ulaghai au unayoshindwa kudhibiti.






## Maswali na Majibu

**Niko kwenye hafla ya kazi iliyoidhinishwa na nilikuwa karibu kutumia kadi yangu ya kampuni kuinunulia timu chakula. Mwenzangu amependekeza nilipe kwa pesa taslimu ili, ninapodai gharama, niweze kusema nilitumia kiasi kikubwa zaidi ili nijipe zawadi kwa kazi ngumu niliyofanya ya kuhakikisha kuwa mradi wetu wa hivi karibuni unafanikiwa. Anasema ukweli, nimefanya kazi kwa bidii sana. Je, ni sawa kufanya hivi?**

Hapana, si sawa Lazima utii Sera ya Kimataifa ya Usafiri na Gharama na kuwa mwadilifu na mwangalifu unapowasilisha madai yako ya usafiri na gharama. Kuwasilisha gharama za uwongo za T&E ni ulaghai dhidi ya Diageo.

**Nimepokea barua pepe inayosema kuwa imetumwa na mteja, akiomba akaunti ya benki yake ibadilishwe. Taarifa ya benki anayoyataja ni sahihi, lakini taarifa ya mawasiliano hayalingani na barua pepe inaonekana kuwa ya kutiliwa shaka. Nina wasiwasi kuwa huenda hili ni jaribio la ulaghai la mtu mwingine dhidi ya Diageo, lakini sijui nifanye nini.**

Ndiyo, huu unaweza kuwa ulaghai dhidi ya Diageo. Ikiwa unashuku chochote, tueleze. Mwambie Msimamizi wako na wakili wako wa ndani wasiwasi wako mara hiyo hiyo. Ikiwa barua pepe inaonekana kuwa ya kutiliwa shaka, unapaswa kufuata mchakato wetu na uripoti jambo hii kwa csi@diageo.com mara hiyo hiyo ili waweze kuchunguza suala hili.

**Mwenzangu mkuu ameniomba nihakikishe kuwa tuna msambazaji mpya atakayetoa rasilimali zote za mauzo (POS) katika soko letu. Niligundua kuwa muuzaji ana jina sawa na mfanyakazi mwenzangu; nilipozungumza naye kuhusu jambo hilo, aliniambia nisimmwambie mtu yeyote. Ameniambia pia nitengeneze PO kwa kuwa tunahitaji kulipa bili HARAKA IWEZEKANAVYO, lakini najua kuwa bado hatujapokea nyenzo zozote mpya Ninapaswa kufanya nini?**

Mwambie Msimamizi wako na wakili wako wa ndani wasiwasi wako mara hiyo hiyo. Huu unaweza kuwa ulaghai wa kutumia cheo vibaya na/au ulaghai wa uwakilishi wa uwongo wa mfanyakazi wa Diageo dhidi ya Diageo. Ulaghai wa ununuzi ni ulaghai wowote unaohusiana na kampuni inayonunua bidhaa au huduma kutoka kwa wahusika wengine. Unaweza kutokea wakati mchakato wa zabuni haujafuatwa kwa usahihi au kukiwa na madai ya malipo ya bidhaa au huduma ambazo hazikutolewa. Ingawa hakuna faida au hasara iliyopatikana katika hali hii, nia ya kupata faida au kusababisha hasara inamaanisha kuwa hii inaweza kuwa mfano wa ulaghai. Ulaghai pia unaweza kuwa changamani na kujumuisha nyanja nyingine, kama vile Mgongano wa Maslahi.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43

# Utakatishaji fedha na kusaidia ukwepaji kodi

**Tunawajibika kupunguza hatari ya utakatishaji fedha na kuwezesha kosa la ukwepaji wa kodi**

Utakatishaji fedha ni utaratibu ambao mapato ya uhalifu yanabadilishwa na kuonekana kuwa ni halali.

Ukwepaji kodi ni kitendo haramu cha kukataa kulipa kodi. Kuwezesha ukwepaji wa kulipa kodi ni kitendo cha mshirika mwingine kumsaidia mtu fulani au shirika kukwepa kulipa kodi.

Sote tunapaswa kuwa macho dhidi ya miamala yenye kutia shaka na maombi na shughuli haramu zinazofanywa na wengine ili tuweze kulinda sifa ya Diageo na kuhakikisha hatutumiwi na wengine kutakatisha fedha au kukwepa kulipa kodi.

## Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kufuata** michakato ya Mjue Mteja Wako na Mjue Mshirika Wako wa Kibiashara (KYBP) iliyoandikwa katika Sera ya Kimataifa ya Kupambana na Ufisadi na Kiwancho cha Mjue Mshirika Wako wa Kibiashara (KYBP)
- **kuandika mabadiliko yoyote** katika maelezo ya mteja au muuzaji, hali au wasifu, na uiambie timu ya fedha ya eneo lako kuhusu taarifa hiyo
- **kufanya biashara** na wateja na washirika wa biashara tuliowachunguza na kuhakikisha kuwa hawana vikwazo (angalia Vikwazo kwenye ukurasa wa 23)
- **kuripoti haraka** kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo, ishara yoyote ya hatari ambayo inaweza kuashiria kwamba mteja au muuzaji huyo anahusika katika utakatishaji fedha au ukwepaji kodi.

**Ishara za hatari zinazoonyesha uwezekano wa utakatishaji fedha na kusaidia ukwepaji kodi**

Sote tunahitaji kuwa macho na shughuli zisizoeleweka, kwa mfano wakati mteja:

- anasita bila sababu maalum kutoa maelezo binafsi au historia ya biashara yake
- anataka kulipa fedha taslimu
- anataka kulipa pesa zaidi au kulipa katika sarafu tofauti na ile iliyoandikwa kwenye ankara
- amesajiliwa katika eneo tofauti na eneo lake kuu la biashara au eneo la kulipa kodi
- anataka kupokea au kulipa fedha kwenye akaunti za benki za nje au katika nchi tofauti na biashara inapofanyika
- anataka kupokea au kulipa fedha kwenye au kutokea akaunti nyingi za benki, au kutumia akaunti ya mtu mwingine.

## Maswali na Majibu

**Mmojawapo wa wateja wetu ameomba kama anaweza kulipa kupitia akaunti tofauti mchanganyiko wa fedha taslimu na hundi. Je, hii ni sawa?**

Unapaswa kutahadhari na muamala huu. Unaibua shaka na pia unaweza kuashiria utakatishaji fedha. Kumbuka kwamba Diageo haiwezi kukubali hundi ya mtu mwingine ambaye siyo mteja wetu. Tafuta ushauri kutoka kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo kabla ya kumjibu mteja.

**Nimepokea taarifa kwamba mmoja wa wasambazaji wetu ameshtakiwa kwa kosa la utakatishaji fedha. Ninapaswa kufanya nini?**

Toa taarifa kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo mara moja na uache kupokea oda ya mzigo kutoka kwa msambazaji huyo. Diageo haiwezi kufanya biashara na watu au kampuni ambazo zimeshtakiwa kwa makosa ya utakatishaji fedha.

**Msambazaji ameuliza kama anaweza kulipwa kwa ajili ya uwekezaji katika uanzishaji na uendelezaji bidhaa kwenye akaunti ya benki nje ya eneo la mkataba wa usambazaji. Je, ninaweza kukubali hili?**

Hapana, hili ni ombi lenye kutia shaka ambalo unapaswa kuripoti mara moja kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo ambaye atahitaji kupewa taarifa zote zinazohusika ili kutoa ushauri, na ikiwa hivyo, jinsi ya kuendeleza uhusiano wa kibiashara na mteja huyo.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43**



# Vikwazo

**Tunaheshimu vikwazo vya kimataifa na vikwazo vingine vya kibiashara**

Kama ilivyoonyeshwa katika maelezo ya kina kwenye Sera ya Kimataifa ya Vikwazo ya Diageo, wakati wa kufanya biashara, tunapaswa kuheshimu sheria zote zinazohusika na kanuni zinazohusu vikwazo vya kimataifa na vikwazo vingine vya kibiashara, huku tukizingatia yanayoendelea katika hatua hizi.

Vikwazo na masharti ya biashara yanatolewa na mamlaka zinazotambulika, zikijumuisha Umoja wa Mataifa, Umoja wa Ulaya na Ofisi ya Udhibiti wa Rasilimali za Kigeni (OFAC) ya Idara ya Hazina ya Marekani. Vikwazo vimewekwa ili kuzuia au kuweka ukomo katika kufanya biashara na nchi fulani na/au pamoja na raia wake, lengo likiwa ni kuimarisha makusudio ya sera mbalimbali za kigeni na usalama wa taifa. Vikwazo vinaweza kuwa vya aina mbalimbali, ikiwemo vikwazo vya kifedha, kufungia rasilimali, kufungiwa kusafiri na kufungiwa kuingiza/kusafirisha bidhaa nje ya nchi.

Hatupaswi kufanya biashara, moja kwa moja au kwa namna nyingine na watu, mashirika, serikali au majimbo ikiwa kufanya hivyo kunakiuka vikwazo vilivyopo. Kwa hiyo ni muhimu kutambua wateja wetu, wauzaji na washirika wengine wa biashara.

## Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kutoanzisha uhusiano** na mshirika wa bishara hadi utakapokuwa na uhakika kuhusu utambulisho wake halisi na mshirika wa biashara awe amechunguzwa, ipasavyo, kupitia Mipango yetu ya KYC/KYBP
- **kupeleka mara hiyo hiyo** 'tahadhari' yoyote au wasiwasi unaojitokeza kwenye mchakato wa kukagua vikwazo kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo na/au Ofisa wa Kuzingatia Vikwazo (SCO), kama inavyofafanuliwa katika Sera ya Kimataifa ya Kupambana na Ufisadi
- **kumjulisha** mwanasheria wako wa ndani wa Diageo na/au SCO ikiwa unafanya biashara au unapanga kufanya biashara kwenye nchi iliyowekewa vikwazo.

## Maswali na Majibu

**Tunaweza kufanya kazi na msambazaji mpya ambaye ana maslahi yasiyohusiana na biashara yetu katika nchi jirani yenye vikwazo. Ninapaswa kufanya nini?**

Hakikisha msambazaji huyo amechunguzwa vikwazo kupitia mchakato wa KYC/KYBP kisha mtaarifu mwanasheria wa ndani wa Diageo na/au SCO mara moja ili waweze kukushauri namna ya kuendelea.

**Ninapaswa kufanya nini ikiwa mmoja kati ya wateja wangu ameonekana kwenye orodha ya waliowekewa vikwazo?**

Ikiwa zana ya kukagua vikwazo itambaini mmoja wa wateja wako waliopo kuwa kwenye orodha hiyo, unapaswa kusitisha kufanya biashara naye mara moja na mjulishe mwanasheria wa ndani wa Diageo na/au SCO.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43**



# *Watu wetu*

*Kuthaminiana* na *kuheshimu* watu wengine:

- Afya, ulinzi na usalama binafsi
- Ubaguzi na unyanyasaji
- Haki za binadamu

# Afya, ulinzi na usalama binafsi

### Sote tuna wajibu wa kuhakikisha mazingira salama ya kazi

Namna mojawapo ya kuonyesha tunathaminiana ni kuhakikisha usalama wetu na wa wale wote walio pamoja nasi. Sote tuna jukumu kubwa la kuhakikisha afya, usalama na ulinzi wa kila mtu anayefanya kazi katika ofisi za Diageo au anayeathiriwa na shughuli zetu, na ni lazima sote tutekeleze wajibu wetu wa kuhakikisha kwamba kila mtu anarudi nyumbani salama, kila siku.

Mazingira salama ni mahali ambapo kila kitu tunachofanya kinaheshimu sheria husika, viwango na utendaji bora katika sehemu za kazi afya, ulinzi na usalama.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kujua na kufuata** sera za ulinzi na usalama na viwango vinavyotumika katika eneo lako na aina ya kazi
- **kutojiingiza** katika mienendo isiyo salama, hali au matendo mabaya ili kuepuka majeraha na magonjwa
- **kutoa haraka taarifa ya ajali**,matukio, koswa koswa, ukiukwaji wa sera, viwango au sheria, au hatari nyingine yoyote ya afya, ulinzi na usalama
- **kukamilisha** mafunzo yoyote yanayohitajika kuhusu afya, usalama na ulinzi
- **kuhakikisha** kwamba Mwongozo wa Diageo wa Upangaji Hafla na Ukabilianaji na Hatari umefuatwa.





## Maswali na Majibu

**Ninandaa hafla kwa ajili ya timu yetu katika ukumbi nje ya eneo la ofisi. Nimeambiwa kwamba natakiwa nifanye tathmini ya usalama na ulinzi. Je, ni muhimu kufanya hivyo?**

Ndiyo, ni muhimu. Wote tuna jukumu la kuhakikisha kuna usalama wa mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wote hata kama biashara inafanywa nje majengo yetu. Kufanya tathmini ya hatari hutusaidia kuhakikisha hilo. Kuhakikisha ukumbi unaendana na viwango vyetu, na kupunguza hatari yoyote itakayojitokeza, itasaidia kulinda wenzako na sifa yetu.

**Nitasafiri kwenda kuona masoko ng'ambo ndani ya wiki chache zijazo. Nina hofu kwamba si salama sana na kwamba ninaweza kuhitaji chanjo. Nifanye nini?**

Kabla ya kusafiri, itabidi uzungumze na mhusika wa afya mahala pa kazi na mhusika wa usalama katika kampuni. Wao watahakikisha kuwa una chanjo zozote, dawa, na habari zote za nchi kuhusu usalama au mafunzo utakayohitaji katika safari yako. Kwa nchi hatarishi zaidi, huwezi kuruhusiwa kununua tiketi mpaka utakapofanya mafunzo ya usalama wakati wa kusafiri na usalama binafsi na pia lazima uwe na afya nzuri kabla ya kusafiri.

**Chapa za Diageo zinaendelea kutangazwa katika hafla mbalimbali, kuanzia matamasha makubwa makubwa na matukio ya michezo, hadi uzinduzi katika kituo kimoja cha usambazaji. Je, ninaweza kupata wapi muongozo kuhusu tukio ninalopanga ili nihakikishe kuwa tukio hilo ni salama na lina ulinzi wa kutosha?**

Unaweza kupata mwongozo kwenye Miongozo ya Diageo ya Upangaji wa Tukio na Ukabilianaji na Hatari na kwa kujaza Hojaji ya Usalama wa Hafla. Kwa ushauri zaidi tafadhali wasiliana na corporate.security@diageo.com.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 43



# Ubaguzi na unyanyasaji

### Tunasherehekea utofauti wetu, kuthaminiana na haturuhusu ubaguzi au unyanyasaji

Sote tuna jukumu muhimu la kujenga mazingira ambayo wafanyakazi, wasambazaji, washirika wa biashara, na wananchi wote wanajisikia kuthaminiwa, wanaheshimiwa, na wana uhuru wa kufanikiwa. Hapa Diageo tunasherehekea utamaduni na uanuwai wa watu binafsi ikiwa kama utamaduni, wetu, na tumeweka sahihi katika Kanuni za Uwezeshaji wa Wanawake za Umoja wa Mataifa. Hatubagui au kuruhusu unyanyasaji kwa misingi ya rangi, dini, rangi, kabila, asili ya taifa, ulemavu, mwelekeo wa kingono, jinsia, utambulisho wa kijinsia, ujinsia au hali ya ndoa.

Kila mmoja wetu anawajibika kuonyesha kiwango cha juu cha uadilifu katika tabia zetu.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kumtendea kila mtu** kwa utu na heshima
- **kusherehekea** tofauti za kitamaduni na za mtu binafsi
- **kukuza** mazingira ya uwazi, ya kushirikiana na ya uaminifu
- **kutovumilia au kutojihusisha** na tabia ya ubaguzi, inayokera au ya kutisha, unyanyasaji, au uchokozi.

#### Nini kinachochukuliwa kuwa ni uonevu?

Mifano ya uonevu inaweza kuwa:

- kufokea, kukejeli, kudhihaki au kuwadhalilisha wengine
- kutoa vitisho na kuonyesha mabavu au kutishia kisaikolojia
- usimamizi uliopitiliza na kutoa maoni mabaya yasiyostahili na /au ya dharau
- matumizi mabaya ya mamlaka au madaraka kwa wale waliopo kwenye nafasi za juu
- kuwatenga wafanyakazi wengine wasihudhurie mikutano/mawasiliano bila sababu za msingi.

#### Tabia ambazo hazitavumiliwa

Zifuatazo ni tabia ambazo hazitavumiliwa:

- unyanyasaji, unyanyasaji kingono au kumchokoza mtu yeyote
- kunyanyapiza, kutishia au kulipiza kisasi dhidi ya mtu yeyote ambaye analalamika kuhusu unyanyasaji au uchokozi
- kutoa madai ya uchokozi, unyanyasaji au unyanyasaji wa kingono kwa kusingizia, au kwa nia mbaya
- kutoa taarifa ya uongo au inayopotosha kwa makusudi wakati wa uchunguzi wowote.



## Maswali na Majibu

**Msimamizi wangu ana vigezo vya juu sana vya utendaji na anataka sisi tufanye kazi vizuri, lakini huwa anatishia sana na wakati mwingine anatukana. Nataka kumsaidia lakini nina wasiwasi kwamba nikimwambia mtu, hali inaweza kuwa mbaya zaidi au hata kuhatarisha kazi yangu. Ninapaswa kufanya nini?**

Tunalenga kuwa na mazingira yanayodumisha uwazi, ushirikiano na uaminifu, na tabia ya uonevu na vitisho haikubaliki, bila kujali hali au cheo cha mtu. Tunatambua kwamba kila mtu ni tofauti na atakuwa na kiwango tofauti cha uvumilivu, cha kwako kitaheshimiwa. Kama huwezi kuongea na meneja wako, unapaswa kuongea na mhusika wa rasilmali watu wa eneo lako au meneja wa meneja wako. Tunakuhakikishia kwamba hatutavumilia ulipizaji kisasi kwa sababu ya kushtaki suala hilo.

**Wakati wa P4G, Kiongozi Wangu alitoa maneno mabaya sana kuhusu utendakazi wangu na mara kwa mara amekuwa akizungumzia udhaifu wangu. Jambo hili si sawa na tabia yake ya uonevu na nilihisi kutishiwa na sikutendewa haki**

Uonevu mahala pa kazi kwa kawaida ni pamoja na (inaweza kuwa zaidi) tabia zisizostahili za mara kwa mara, kwa namna yoyote ile, iwe kwa maneno au kwa vitendo, kisaikolojia au vinginevyo, unaofanywa na mtu mmoja au zaidi dhidi ya mwingine au wengine. Tukio moja linaweza kutokea na kuhisiwa kama kitendo cha kuvunjiwa heshima kazini lakini linaweza lisiwe la uonevu hadi pale litakapokuwa linatokea mara kwa mara.

Uchokozi kazini haujumuishi ukosoaji halali au wa wenye lengo la kujenga utendaji kazi au tabia ya mtu, wala kuwaomba wafanyakazi kutekeleza majukumu yao. Hii ni sehemu ya mchakato wa ajira na usimamizi wa kawaida na haipaswi kutafsiriwa tofauti. Hata hivyo, ikiwa mazungumzo ya utendakazi kama ilivyotajwa katika mfano huu, yanakufanya ujisikie vibaya au kuhuzunika, bado tunakuhimiza kutoa taarifa ya jambo hili kupitia njia zinazojulikana.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 44

# Haki za binadamu

### Tunataka kuwa na mchango mzuri kwenye masuala ya haki za binadamu na za kijamii

Tunatambua wajibu wetu wa kuheshimu na kukuza viwango vya kimataifa za haki za binadamu katika shughuli zetu. Diageo ina jukumu la kutenda kwa mujibu wa Kanuni za Mwongozo za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu. Sera zetu zinatokana na Tamko la Kanuni za Msingi na Haki ya Kufanya Kazi la Shirika la Kazi Duniani (ILO), Haki za Watoto na Kanuni za Biashara, Kanuni za Kimataifa za LGBTI za Kufanya Biashara za Umoja wa Mataifa, Kanuni za Kuwezesha Wanawake za Umoja wa Mataifa na Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa, ambao kama nchi tumeusaini.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kumtendea kila mtu** kwa utu na heshima
- **kusherehekea** tofauti za kitamaduni na za mtu binafsi
- **kutovumilia au kutojihusisha** na tabia ya ubaguzi, inayokera au ya kutisha, unyanyasaji, au uchokozi
- **kutofanya kazi kimakusudi** na mtu yeyote anayejulikana au anayeshukiwa kuwa anatenda vitendo vinavyokiuka haki za binadamu za mtu yeyote kama vile kutotii sheria za mishahara na saa za kufanya kazi, au kutoruhusu unyanyasaji wa watoto, au kuheshimu uamuzi wa kujiunga au kutojiunga na muungano wa wafanyakazi
- **kuhakikisha kuwa washirika, wasambazaji na washirika wengine** unaofanya kazi nao **wanafuata viwango sawa** vinavyohusiana na hakli za binadamu na wanazingatia kanuni katika Ushirikiano wetu wa Kimataifa na Kiwango cha Wasambazaji

## Maswali na Majibu

**Nimegundua kwamba mmoja wa wasambazaji wetu anapunja mishahara. Mkataba wetu na msambazaji hautaangaliwa upya hadi mwaka ujao, lakini sitaki kupuuza suala hilo. Ninapaswa kufanya nini?**

Diageo inatarajia kuona wasambazaji bidhaa na washirika wa biashara wakilipa mishahara stahiki kulingana viwango vya sekta zao. Unapaswa kushiriki wasiwasi wako na msimamizi wako na timu ya manunuzi na mkubaliane hatua sahihi za kuchukua.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma,** **tazama ukurasa wa 44**






# *Mali Zetu* na taarifa

## Kuwa kama wamiliki

Usimamizi wa taarifa na usalama
Usiri wa data na taarifa binafsi
Mali na rasilimali za kampuni
Rekodi za biashara

# Usimamizi wa taarifa na usalama

## Sote tuna wajibu wa kulinda na kusimamia taarifa za Diageo

Taarifa za Diageo ni rasilimali zenye thamani, na sote hatuna budi kusaidia kulinda na kuzisimamia ipasavyo. Iwapo taarifa za siri au za siri sana zitatolewa nje ya Diageo, zinaweza kuharibu ushindani wetu, kuathiri matokeo yetu ya kifedha na kuharibu sifa yetu. Ambapo tumekabidhiwa na mshiriki wetu maelezo ya siri ya biashara ni lazima kuyalinda na kuyasimamia kama ipasavyo.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **utumie nywila ndefu**, na uitunze pamoja na taarifa zako binafsi sehemu salama na ya siri
- **kutunza** taarifa zote za Diageo zinazoonekana na umma, kwa kutumia uainishaji wa Jumla, Siri au Siri Sana, kama inavyoelezwa ikatika mwongozo wetu wa Viwango vya Utunzaji Taarifa
- **kujadili tu na kisha utoe idhini ya kupata** taarifa ya siri au siri sana kwa wale ambao wanazihitaji ili kufanya kazi zao na hakikisha kwamba taarifa yoyote ya siri au siri sana ina vidhibiti muafaka hadi kufikiwa.
- **kuweka taarifa yote**, kuwa ya siri au vinginevyo, ikiwa imepangwa vyema, inayoweza kutambulika na kufikiwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Taarifa ya Mahali na uitupe kwa usalama kwa mujibu wa kazi yako au orodha ya mali ya taarifa ya soko
- **unapokuwa katika sehemu ya umma au biashara** (mfano mikahawa, viwanja vya ndege au vituo vya treni), usifanyie kazi kitu chochote ambacho, kuna hatari taarifa hiyo inaweza kuibwa na kutolewa, na muulize mmiliki wa biashara jina la mtandao na nenosiri ili kuhakikisha unaingia kwenye mtandao halali wa Wi-Fi.
- **kuwa mwangalifu hasa** wakati watu wanapojiunga, wanapohama au wanapoondoka katika kampuni hakikisha uwezekano wao wa kupata taarifa ni sahihi na muafaka, kwamba mtu anapewa au kuondolewa mifumo hiyo kadiri inavyotakiwa.

# Maswali na Majibu

**Naamini kwamba taarifa zimeonekana bila idhini. Je, inapaswa kufanya nini?**

Matukio yote ya usalama wa taarifa yanapaswa kuripotiwa kwa csi@diageo.com mara hiyo hiyo. Timu ya kushughulikia tukio la ulinzi wa kompyuta itaanzisha mchakato wa kushughulikia suala hilo ili kuchunguza na kudhibiti tatizo na kuchukua hatua zaidi ili kudhibiti hatari kwa ufanisi. Pale ambapo taarifa binafsi zimeingiliwa toa ripoti mara moja kwa kuwa huenda tukawa na matakwa ya kiudhibiti ya kutoa taarifa ndani ya muda mfupi sana mfano, saa 72.

**Nitakuwa nasafiri sana katika wiki chache zijazo na sitapendelea kuchukua kipakatalishi changu. Najua nitaweza kusoma barua pepe zangu binafsi kwenye mtandao je, ninaweza kuwezesha barua pepe zangu kutoka Diageo kikashani mwangu zije moja kwa moja kwenye barua pepe yangu binafsi? Hapana, haupaswi kuwezesha barua pepe za Diageo zitumwe moja kwa moja kwenye barua pepe yako binafsi.**

Hii inaweza kuhatarisha usalama wa taarifa zetu, kwa sababu barua pepe zinaweza kuwa na taarifa za siri ambazo kwa kawaida zinalindwa na mifumo ya usalama wa kidijitali ya Diageo, ambayo haipo kwenye barua pepe yako binafsi.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 44**





### Je, taarifa ya siri kabisa ni ipi?

Rasilimali taarifa ni siri ikiwa kutolewa kwake bila idhini kunaweza kusababisha madhara makubwa au madhara kwa maslahi ya Diageo au ikiwa imezuiliwa kisheria au na kanuni isitolewe. Njia moja ya kutofautisha kati ya taarifa ya siri na ya siri sana ni kuangalia kiwango cha athari kwa Diageo iwapo taarifa hiyo imetolewa. Ufichuaji wa taarifa ya siri sana huenda, kwa mfano, ukaathiri sifa ya Diageo au bei ya hisa lakini siyo mara zote linaweza kuwa tatizo kwa ufichuaji wa taarifa za siri.

Mifano ya taarifa za siri sana:

- siri za biashara, kama taarifa za mapishi na usindikaji pombe
- taarifa nyeti zinazomtambulisha mtu.

### Je, taarifa ya siri ni ipi?

Rasilimali taarifa ni siri ikiwa kutolewa kwake bila idhini (hata ndani ya Diageo) kunaweza kusababisha madhara au kuvuruga maslahi ya Diageo au kampuni tanzu zake.

Mifano ya taarifa ya siri ni:

- taarifa za fedha zisizo za umma
- mipango ya biashara, makadirio au mikakati
- masoko, ugunduzi na mipango ya shughuli za matangazo
- orodha ya bei na orodha ya wateja
- taarifa binafsi zisizo nyeti kuhusu wafanyakazi wetu, wateja, wasambazaji, wanunuzi na wengineo (tazama maelezo ya siri na taarifa binafsi katika ukurasa wa 32)
- data za mishahara.

### Orodha za mali ya taarifa na umiliki halali

Tunatakiwa kuhifadhi kwa usalama aina fulani za taarifa kwa muda maalumu. Vipindi hivi vya kuhifadhi nyaraka vimeandikwa kwenye orodha ya taarifa za rasilimali nyaraka. Kila timu inapaswa kuwa na 'mtunza taarifa' ambaye anaweza kukueleza jinsi ya kupata taarifa zinazohusiana na timu yako.

Mara kwa mara inaweza kuwa jambo muhimu kusimamisha kuendelea kuwepo vipindi maalum vilivyotajwa katika orodha ya maelezo ya siri na kuendelea kuhifadhi maelezo hayo kwa muda mrefu kwa ajili ya uchunguzi, ukaguzi au madai. Hii inajulikana kama 'kushikilia kisheria', na mwanasheria wa Diageo atakuambia nini unachohitaji kufanya kama wewe ukijikuta katika hali hii.

# Usiri wa data na taarifa binafsi

## Tunaheshimu taarifa binafsi na kuwajibikia kuzitunza vizuri

Katika kufanya kazi zetu, baadhi yetu tutakuwa na kuona taarifa binafsi kuhusu wenzetu, wateja, wauzaji, wasambazaji, na watu wengine. Ni muhimu kwamba tuheshimu ufaragha wa watu wote na kulinda taarifa kwa mujibu wa maadili yetu, sheria zinazotumika na kudumisha faragha kama haki ya binadamu.

Taarifa nyeti ya binafsi inayohusiana na afya ya mtu, vipimo vya kibayolojia, rangi, kabila, maoni ya kisiasa, imani ya kimaadili na kidini, maisha ya ngono, au shughuli za uhalifu zinatakiwa kuhifadhiwa kwa uangalifu.

### Fanya jambo sahihi

Wakati wewe, au wengine kwa niaba yetu wanakusanya, kushikilia au kuchakata taarifa zozote za kibinafsi lazima uhakikishe:

- **kuwa unajua bayana** kuhusu jinsi data ya kibinafsi inavyotumiwa, na unazingatia notisi zetu za faragha.
- **kuwa unakusanya tu data inayotosha** na inayohusu madhumuni yako ya kuitumia
- **kuwa unakusanya tu unachohitaji** na kwa muda unaohitaji kukitumia
- **kuwa unasasisha data ya kibinafsi**, unasahihisha taarifa isiyo sahihi unapoombwa ufanye hivyo
- **kuwa unalinda na kuweka** data ya kibinafsi kwa usiri
- **kuwa daima, unazingatia hatari** kwa watu binafsi katika kutumia data zao za kibinafsi na kuchukua hatua za kupunguza hatari.
- **kuwa unaripoti mara hiyo hiyo** tukio lolote linalowezekana au la kweli la ukiukaji linalohusisha data ya kibinafsi kwa CSI@diageo.com, na kutumia pia Afisa wa Diageo wa Faragha ya Data ya kimataifa barua pepe kwa DPO@diageo.com
- **kuwa kama unatumia wahusika wengine** ambao wanamiliki, kukusanya au kuchakata taarifa za kibinafsi kwa niaba ya Diageo, unafanya tathmini ya hatari ya faragha kwa kushirikiana na idara ya ununuzi na timu kuu ya faragha kabla ya kujihusisha katika uhusiano
- **kuwa huhamishi data nje ya nchi** ambayo inakusanywa bila ushauri kutoka kwa kiongozi wako wa Faragha au wakili wa ndani wa Diageo.

### Kushughulikia na kutumia taarifa binafsi

Taarifa binafsi ni lazima:

- iwe wazi na uwaambie watu unachonuia kutumia data ya kibinafsi
- uitumie jinsi ulivyosema utafanya
- ukusanye tu kile unachohitaji, kidogo ni zaidi!
- uiweke sahihi, muhimu na ya kisasa
- uihifadhi kwa muda unaoihitaji
- utunze utakachopata
- wajibika.

← ⌂ →

## Maswali na Majibu

**Nataka kuipa kazi kampuni iendeshe mradi wa ubunifu wa 'big data' kwenye mtandao wa intaneti ili tupate ufahamu kitabia. Je, tutathmini vipi hatari za usiri wa data?**

Wakati unapopanga mradi unaombatana na ukusanyaji, au uchakataji wa data binafsi kwa madhumuni ya uchanganuzi au 'kuweka wasifu', unapaswa kutafuta ushauri wa kisheria kutoka kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo na utume barua pepe kwa timu kuu ya faragha katika DataPrivacyTeam@Diageo.com ambao watasaidia kufanya tathmini ya faragha nawe. Unapasawa kufanya hivi hata unapoomba shirika lishughulikie taarifa za kibinafsi kwa niaba yetu.

**Nilipata lahajedwali ya excel ambayo haijalindwa kwenye mfumo wetu, ikiwa na taarifa za kibinafsi za baadhi ya wafanyakazi ambazo sistahili kuona. Najua kwamba tunahitaji kulinda taarifa hii kwa nenosiri na kuzuia mtu kuifikia, lakini sina uhakika nifanye nini.**

Uko sahihi, tunahitaji kulinda maelezo haya kwa makini. Ripoti tukio hili la data ya kibinafsi kwa csi@diageo.com mara hiyo hiyo ili waweze kuchunguza suala hili na kuhakikisha kuwa kuna vidhibiti vya usalama wa kiufundi na shirika vya kutosha.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 44**

← ⌂ →



# Mali ya kampuni na rasilimali

## Sote tuna wajibu wa kulinda mali na rasilimali za kampuni

Sote tumekabidhiwa mali na rasilimali za Diageo, kuanzia hakimiliki za Diageo hadi vifaa vya kampuni (kama vile vifaa simu, kompyuta, mashine za uchapishaji, mashine za kutolea nakala na magari ya kampuni), fedha za kampuni, majengo, na taarifa, ambazo zinahifadhiwa kwenye kifaa binafsi. Wakati mwingine tunaweza kukabidhiwa mali za mashirika mengine, au za watu binafsi au za washirika wa biashara.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kutumia tu** mali na rasilimali za Diageo kwa njia inayofaa, halali na inayofaa, na usithubutu kutumia, kuchukua, kuuza, kukopesha, kukopa au kutoa chochote bila idhini ifaayo
- **kuwajibika kila wakati** na kutenda ukizingatia amslahi ya Diageo unapotumia pesa za Diageo au unapotoa ahadi za kifedha kwa niaba ya kampuni
- **kutii** Sera ya Kimataifa ya Usafiri na Gharama na konyesha uadilifu na uangalifu unapowasilisha madai yako ya usafiri na gharama, na unapoidhinisha madai ya watu wengine.
- **kuheshimu mali** na rasilimali za mashirika mengine na washirika wetu wa kibiashara, na usiwahi kupakua, kunakili, kusambaza, kuchapisha kwenye tovuti au kutumia nyenzo zozote zinazolindwa na hakimiliki ya mtu mwingine au shirika bila kuomba ruhusa yao
- **kushauriana na wakili wako wa IP wa Diageo** ikiwa unahusika katika kutengeneza bidhaa, teknolojia, utangazaji au kampeni zozote za utangazaji, ili uhakikishe kuwa haki zetu za uvumbuzi zinalindwa ipasavyo
- **kuelewa kuwa kazi yako** (kama vile barua pepe, mawasiliano kupitia mkondo wowote na maudhui unayotengeneza) ni ya Diageo na, inaporuhusiwa kisheria, yanaweza kufikiwa na kutumiwa na kampuni, hata baada ya kuondoka kwako kwenye kampuni.

### Hakimiliki ni nini?

Taarifa binafsi ni lazima ziwe:

- **chapa zetu za biashara** ambazo hulinda bidhaa zetu
- **leseni** zinazolinda uvumbuzi wetu, kama vile teknolojia yetu ya kipekee na mbinu za uzalishaji
- **hakimiliki na ubunifu** ambao unalinda mawasiliano yetu, vifaa vya matangazo na masoko, na chupa na vifurushi vyetu vya kipekee
- **siri za biashara yetu**, kama vile resipe na taratibu za kusindika pombe.

## Maswali na Majibu

**Naweza kumtumia barua pepe rafiki yangu tukutane baa baada ya kazi nikitumia barua pepe yangu ya Diageo?**

Ndiyo, unaweza kutumia barua pepe yako ya Diageo kama barua pepe yako binafsi, ilimradi ufanye hivyo mara chache tu. Hata hivyo, kumbuka kuwa Diageo inaweza kuiona na kuitumia kwa madhumuni yake halali ya kibiashara kulingana na sera zetu na sheria za eneo husika.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 44**

# Rekodi za biashara

**Diageo imejizatiti kuwa na utendaji madhubuti katika maeneo yote ya biashara yetu. Ni lazima sote tuhakikishe kumbukumbu za biashara zetu zimekamilika, ni sahihi, na kuidhinishwa ipasavyo**

Kila mtu ana wajibu wa kuhakikisha kwamba rekodi zote tulizotayarisha kwa niaba ya Diageo ni za kweli na ni sahihi.

Kumbukumbu sahihi inahitajika kutoa taarifa ya fedha na isiyo ya kifedha ili kukidhi masharti ya kisheria. Udanganyifu katika rekodi hizo unaweza, wakati mwingine, kuwa utapeli au kosa la jinai na laweza kusababisha adhabu kwako na kwa Diageo. Pamoja na hayo, rekodi sahihi zinatusaidia kufanya maamuzi kuhusu biashara yetu na ni muhimu katika kutimiza majukumu yetu kwa wanahisa wetu, mamlaka, na watu wengine. Diageo haiwezi kukubali au kupuuza jitihada zinazofanywa kuhamisha mauzo kutoka kipindi kimoja kwenda kingine bila kuwepo sababu ya kibiashara ya kweli, isiyoepukika.

## Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kuhakikisha** kwamba kumbukumbu zote za biashara ni sahihi, zinaendana na masharti na sheria zetu za kampuni
- **kutofanya** au kuidhinisha shughuli yoyote iliyolengwa katika vipindi vya mwisho wa mwaka bila sababu ya msingi kwa kuwa hizi huweza kuashiria shauku ya kuhamisha mauzo au gharama ili kubadilisha faida kwa kughushi katika vipindi vya kuripoti. Mifano inaweza kujumuisha kubadilisha au kuongeza masharti ya malipo kwa mteja fulani, kubadilisha sera ya kurudisha bidhaa zilizonunuliwa, kutoa masharti ya mkopo maalumu au yasiyokuwa ya kawaida kwa mteja au kutoa ghala la kuhifadhi "bila malipo" au "kwa ruzuku" hadi bidhaa itakapotolewa mwezi unaofuata.
- **kuhakikisha** kwamba masharti yote ya mikataba kwa niaba ya Diageo yanaidhinishwa na mtu sahihi – unaweza kupata maelezo katika Mwongozo wa Mamlaka kutoka Kampuni Mama (Group SoA) au katika Mwongozo wa Mamlaka katika nchi yako.
- **kuripoti** kwa kiongozi wa juu kiwango chochote kisicho cha kawaida cha bidhaa sokoni mwisho wa mwezi kama sehemu ya mchakato wa kuanika mambo mabaya yanaoendelea
- **kutunza** rekodi za biashara kwa kuzingatia kipindi husika cha kuyatunza kwa kufuatilia masharti ya soko la eneo lako kitengo chako cha biashara (tazama ukurasa wa 31)
- **kushauriana** na wafanyakazi wenzako wa fedha na wa kisheria ikiwa una maswali yoyote kuhusu vitendo au mipango ya mwisho wa kipindi iliyopendekezwa na kutumiwa na kampuni, hata baada ya kuondoka
- **kutii** Sera ya Usafiri na Gharama za Ulimwenguni ambayo inaweka mahitaji muhimu ili kuwapa wafanyakazi wa Diageo kwa ufanisi na gharama nafuu usafiri na malazi, huku ikihakikisha kuwa huduma hizi zinakidhi viwango vya chini vya usalama, uendelevu, huduma na bei.

### Rekodi za biashara ni nini?

Rekodi za biashara ni hati yoyote au mawasiliano yaliyofanywa au kupokewa wakati wa shughuli za kibiashara. Hii ina maana taarifa za fedha na akaunti, na pia rekodi kama vile za mawasilisho, mipango ya biashara, nyaraka za kisheria, matokeo ya utafiti wowote au majaribio, na nyaraka za Rasilimali Watu pamoja na nyaraka za kusafiria-na gharama zinazohusiana.

# Maswali na Majibu

**Tunakaribia mwisho wa mwaka wetu wa kifedha na meneja wangu ameniomba niwape motisha wateja ili wanunue kiasi kikubwa cha bidhaa sasa hivi na sio kipindi kinachofuata. Kulingana na takwimu za awali za mauzo, wateja hawa hawataweza kuuza haya yote kwa wateja mwaka huu. Je, hii ni sawa?**

Hapana, hii inaitwa 'kupandisha mauzo', ni zoezi lenye kusudi la kutaka kuhamisha mauzo kutoka kipindi kimoja hadi kingine cha fedha, jambo lisilokubalika. Kunaweza kuwa na wakati mwafaka ambapo sisi na wateja wetu tukiamini kuwa ni sahihi ili kuongeza viwango vya hisa katika biashara, nje ya mwendo wa kawaida wa biashara - kwa mfano, manunuzi yaliyofanywa kabla ya ongezeko lilotarajiwa la kodi, gharama za kufunga bidhaa, au kabla ya shughuli kubwa ya utangazaji au kabla ya tangazo la ongezeko la bei. Hata hivyo, shughuli kama hizo daima husukumwa na sababu zilizo wazi, halisi na za kibiashara. Zungumza na mwanasheria wa Diageo na timu yako ya fedha ikiwa unahitaji ushauri.

**Ninataka kuandikisha mkataba wa miaka mitano na msambazaji mpya. Je, ninahitaji vibali gani?**

Kwa kuwa mkataba huu ni wa kipindi cha miaka mitano, unahitaji kuchukuliwa kama mkataba mkubwa wa manunuzi. Tafadhali angalia Mwongozo wa Mamlaka kutoka Kampuni Mama, (Group SoA) ambayo inataja masharti maalum kwa ajili ya mchakato huu wa kuomba idhini. Nchi nyingi pia zina Mwongozo wa Mamlaka ya mahali husika, kwa hiyo tafadhali zungumza na msimamizi wako wa fedha wa mahali ili kuhakikisha matakwa ya mahali husika pia yanafuatwa. Aidha, kwa kuwa huyu ni msambazaji mpya, utapaswa kuhakikisha kwamba matakwa katika Kiwango cha Mjue Mshirika Wako wa Biashara yanafuatwa.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma,** **tazama ukurasa wa 44**




# *Jamii na washirika* wetu

## Tunajivunia na mahusiano tunayoyaendeleza


Ubora

Uendelevu wa Mwanzo hadi Mwisho

Michango ya hisani

Mawasiliano ya nje na mitandao ya kijamii

Mahusiano na wateja, wasambazaji bidhaa na washirika wengine wa biashara

# Ubora

### Ubora wa bidhaa zetu ni jambo muhimu sana katika mauzo, leo, na hata siku zijazo

Sisi ni viongozi tuliosimamia bidhaa nyingi za vinywaji ambavyo vyenye mafanikio makubwa na kuheshimika duniani, na tunapenda sana kuwapatia wateja bidhaa bora iwezekanavyo. Sote tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba tunaendeleza na kukuza sifa za bidhaa zetu kwa kutoa viwango bora katika maeneo yote ya biashara yetu, kuanzia viungo vyetu hadi ufungaji; kuanzia huduma kwa wateja hadi ubunifu wa bidhaa, na katika mlolongo wetu wa kuuza.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kuhakikisha** kwamba bidhaa zetu na bidhaa zingine zinazohusiana zinatumika kwa usalama, zinafuata kanuni zote zinazohusika, hazina kasoro ya ufungaji, zinatumika kikamilifu na zina ladha nzuri wakati wote
- **kuhakikisha** ubunifu na miundo yote ya ufungaji na mabadiliko mengine katika bidhaa yamefanyika vizuri kwa mujibu wa viwango vyetu vya ubora
- **kuhakikisha** kwamba washirika wa biashara, ikiwa ni pamoja na wachuuzi na wazalishaji wengine, wanafanya kazi kulingana na Sera yetu ya Ubora wa Kimataifa
- **kufuata** mfumo wa usimamizi wa ubora wa kitengo chako cha biashara.



## Maswali na Majibu

**Hivi karibuni kaka yangu alinunua chupa ya Smirnoff Red, akaniambia haifunguki. Ninapaswa kufanya nini?**

Tuna wajibu wa kujibu mara moja kama kuna wasiwasi kuhusu ubora wa bidhaa au usalama, hata kama itabidi kurudisha bidhaa kiwandani. Unapaswa kuripoti suala hilo mara moja kwa timu yako ya usambazaji.

**Ninafanya kazi katika idara ya uzalishaji na nimeona bidhaa mbovu ambazo haziendani na viwango vyetu. Nimeongea na msimamizi wangu lakini kaniambia nisiwe na wasiwasi kwa sababu makosa ni madogo sana. Je, amesema ukweli?**

Hapana. Tunajitahidi kufikia viwango vya ubora wa juu kwa kila kitu tunachofanya. Tunataka wateja wetu wafurahishwe na bidhaa bora na hata kosa dogo linaweza kuathiri juhudi zetu na kuweza kuharibu sifa yetu. Unapaswa kurudi kwa msimamizi wako wa wafanyakazi na kupinga maamuzi yake na kama ataendelea kukataa ni lazima kuzungumza na msimamizi wako.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 44





# *Uendelevu* wa kuanzia nafaka hadi glasini

### Tumejitolea kuhifadhi maliasili kwenye ambayo sote tunaitegemea

Mafanikio yetu ya kudumu ya muda mrefu yanategemea watu na sayari inayotuzunguka. Tunatambua kwamba umaskini, ukosefu wa usawa, mabadiliko ya hali ya hewa, matatizo ya maji, upotevu wa bayoanuwai na changamoto nyinginezo zinatishia mazingira na ustawi wa jamii.

Society 2030: Spirit of Progress ni mpango wa utekelezaji wa miaka 10 wa Diageo ili kusaidia kuunda ulimwengu jumuishi na endelevu zaidi. Malengo Yetu ya Society 2030 yanazingatia mpango huu wa utekelezaji wa miaka 10, unaojenga urithi wa waanzilishi wetu ili kuleta athari chanya katika kampuni yetu na jumuiya yetu na kwa ajili ya jamii.

Sera yetu ya Kimataifa ya Mazingira ni sehemu ya Mfumo wa Kanuni ya Maadili ya Biashara ya Diageo na inaweka wazi wajibu na matarajio yetu ya kudhibiti athari ndani na nje ya mazingira. Sera ya Mazingira inatumika kwa wasimamizi na wafanyikazi wote wa Diageo, mashirika yote ya wahusika wengine, ikiwa ni pamoja na wasambazaji na wakandarasi.

Chapa zetu zote, masoko na maeneo ya usambazaji yanalenga kupunguza athari mbaya kwa Mazingira na kutafuta fursa za kufanilisha uendelevu wa mazingira. Mwingiliano wetu na ulimwengu wa asili ni changamano na tutaendelea kukuza mtazamo kamili wa uendelevu, unaotegemezwa na kujitolea kwetu kwa Kufanya Biashara kwa Njia Inayofaa kuanzia Mwanzo hadi Mwisho.

Sehemu ya 'Mahali pa kupata taarifa zaidi' ya Sera yetu ya Kimataifa ya Mazingira ina viungo vya nyenzo muhimu na mafunzo kwa wafanyakazi wa ndani.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kushughulikia** na shughuli zisizokuwa endelevu unapoziona, ikiwa ni pamoja na watu au michakato inayotumia maji vibaya, nishati na rasilimali zingine; kama uchakataji taka hautafanywa kwa ufanisi (ikiwemo ufungaji, mchakato wa kuzalisha bidhaa na vifaa vinavyofikia muda wa mwisho wa kutumika)
- **kuwapa changamoto** wafanyakazi wenzako wanaoshindwa kuzingatia athari za mazingira katika maamuzi ya biashara na kuwa na ujasiri wa kuripoti wasiwasi
- **kuhusika** na kuunga mkono juhudi za miradi ya ndani, kama vile fursa za kujitolea, usafiri unaotumia nishati mbadala ya kijani na kuhifadhi nishati
- **kuhakikisha** kwamba unatoa taarifa mara hiyo hiyo kuhusu hatari za mazingira, au hali yoyote ambayo si sawa kwa msimamizi wako, kupitia Speak Up
- **kutafuta fursa** za kushirikiana na wasambazaji wetu ili kupunguza athari zao kwa mazingira
- **kuchukua hatua** ya kujifunza na kuimarisha ujuzi wako kuhusu mbinu endelevu ndani na nje ya biashara.

## Maswali na Majibu

**Ninahitaji mwongozo mahususi kuhusu uendelevu wa Mwanzo hadi Mwisho kwa ajili ya shughuli zetu na ugavi – ninaweza kupata wapi hii?**

Kurasa za mazingira za tovuti yetu ya sera huwapa wadau wa ndani nyenzo na mwongozo ili kusaidia kutekeleza mkakati wetu. Maudhui yaliyo kwenye tovuti yamepangwa katika maeneo ya mada: Hakikisha hadi ulimwengu wa Kaboni kupungua, Hifadhi Maji kwa Uhai na Uwe Endelevu kwa Ubunifu.

**Mmoja wa wateja wetu anauliza maswali kuhusu uendelevu wa Mwanzo hadi Mwisho – ninaweza kupata wapi taarifa za kunisaidia kujibu?**

Kuna 'vyanzo salama' kadhaa vya taarifa ambayo vinaweza kutumika kujibu maswali mengi, haya tayari yako kwa umma: Kurasa za Society 2030 kwenye tovuti yetu na Sera ya Kimataifa ya Mazingira zinaeleza malengo yetu, kwa kutumia mifano. Ripoti ya Kila Mwaka na Kielezo cha Kuripoti cha ESG hutoa maelezo ya ziada kuhusu jinsi tunavyowasilisha Society 2030 yetu: Malengo ya Spirit of Progress. Ikiwa huwezi kupata taarifa unazohitaji katika maeneo haya na unahitaji usaidizi zaidi, tafadhali wasiliana na: spiritofprogress@diageo.com

**Tunafanya kazi fulani ya ajabu ya uendelevu katika kazi yangu - Je, ninaweza kuwasilianaje hili kutoka nje?**

Ni muhimu kwamba taarifa tunazotoa nje zidhibitiwe ili kuhakikisha uhalali na kuepuka kutolewa kwa taarifa za uwongo. Maudhui yote **lazima** yaidhinishwe na CR na idara ya kisheria kabla ya kutolewa. Mwongozo mahususi kuhusu jinsi ya kutengeneza taarifa za nje zinazozingatia unaweza kupatikana katika hati ya Mwongozo wa Madai Endelevu. Ikiwa huwezi kupata taarifa unazohitaji katika mwongozo huu tafadhali wasiliana na mwanasheria wako kwa usaidizi.

Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 44

# Michango kwa vyama vya kujitolea

### Tunataka kutekeleza jukumu na kushirikiana na jamii zetu

Biashara yetu inaleta mabadiliko katika maisha ya mamilioni ya watu duniani kote, na tunaamini kwamba nchi na jamii ambayo sisi tunafanya kazi wananufaika na uwepo wetu. Kufanya michango kwa ajili ya vyama vya kujitolea ni njia mojawapo ambayo Diageo inawza kuleta mabadiliko.

Tunafanya kazi kwa uadilifu wakati tukifanya mchango kwa vyama vya kujitolea, kuhakikisha michango yetu yote iko wazi, na inafanywa kufuatana na sheria husika, na haitolewi kwa ajili ya kujaribu kuendesha biashara nje ya sheria, kwa niaba ya Diageo. Tunatoa mchango wetu kwa vyama vya kujitolea na kuhakikisha kwamba michango yetu inatumika kwa ajili ya shughuli za vyama hivyo.

Kabla ya kutoa mchango kwa niaba ya Diageo, bila kujali thamani, lazima upate idhini, kama inavyoelezwa hapo chini. Hii ni kuhakikisha kwamba hakuna hatari ya mchango halisi kufikiriwa kama ni kitu kingine, kama vile rushwa. Kama afisa wa serikali (tazama ufafanuzi ukurasa wa 17) au mtu yeyote kwa niaba ya serikali anashawishi, au anaomba msaada kwa ajili ya vyama vya kujitolea au anahusiana kwa njia fulani na taasisi ambayo inahusiana na Diageo, lazima umuarifu afisa mahusiano na mwanasheria wa Diageo.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kupata kibali** kutoka kwa idara ya mahusiano katika kampuni kabla ya kutoa mchango wowote wa msaada kwa niaba ya Diageo
- **kupata kibali** kutoka kwa mwanasheria wa ndani wa Diageo kabla ya kutoa mchango wowote wa misaada ambao unahusisha afisa wa serikali
- **kuandika michango ya misaada** katika mifumo husika ya uhasibu ya Diageo na kumbukumbu, kulingana na vigezo vya utoaji misaada nchini mwako.

# Maswali na Majibu

**Tumeombwa kudhamini meza kisha tutoe bidhaa katika hafla ya kuchangisha fedha. Tunaweza kufanya hivyo?**

Ndiyo unaweza, lakini, kama ilivyo kwa misaada yote tunayotoa, mnapaswa kuhakikisha kuwa shirika litakalopokea msaada huo linakidhi vigezo. Kabla ya kuendelea, hakikisha una kibali kutoka idara ya mahusiano kisha nakili malipo ya meza, na mchango wa bidhaa, kwa mujibu wa taratibu za nchi husika kulingana na vigezo vya michango ya hisani.

**Mimi binafsi nahusika kwenye mpango wa kusaidia shule za mahali nilipo katika kuboresha ujuzi wa watoto kusoma. Kwa sasa wanatafuta watu wapya wa kujitolea na nafikiria kuwaomba wenzangu kazini ikiwa wangependa kushiriki. Je, hii ni sawa?**

Unaweza bila shaka kuwaambia wenzako washiriki, lakini kwa vile si sehemu ya mpango wa Diageo, msifanye wakati wa kazi. Sisi kuhimiza wafanyakazi kujiingiza sababu ambazo ni muhimu kwao na jamii zao, lakini ni lazima kuwa na hasa makini kwamba matendo yetu si vibaya kama jaribio la soko la bidhaa zetu kwa wale walio chini ya umri wa kisheria kununua. Kwa ushauri zaidi, tafadhali zungumza na idara ya mahusiano ya kampuni.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 44**






### Je, Diageo hutoa michango katika mashirika ya aina gani?

Tunasaidia mashirika ya misaada, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), mashirika yasiyojihusisha na shughuli za kujifaidisha ambayo yanatoa michango kwa madhumuni ya kufaidisha umma kwa ujumla. Timu yako ya masuala ya mahusiano itakupa ushauri.

### Je, mchango wa hisani (msaada) unaotolewa na kampuni ndiyo upi?

Diageo inaunga mkono shughuli za kutoa misaada na inaweza kuja kwa njia nyingi, ambayo inaweza kuwa fedha, kutoa bidhaa zetu, au namna nyingine kama vile kutoa nguo na hata muda kutekeleza jambo.

### Shughuli za uhisani za mtu binafsi

Wakati mwingine wafanyakazi huomba wafanyakazi wenzao kuwasaidia shughuli zao binafsi za utoaji misaada, kwa mfano, kuwadhamini kukimbia riadha, kuchangisha fedha kwa kuandaa keki nyumbani, au kukusanya vidubwasha visivyotumika. Ikiwa ni shughuli ambayo Diageo haihusiki nayo, basi haichukuliwi kama mchango wa kampuni, na haitafuata utaratibu uliotajwa katika sehemu hii. Hata hivyo, iwapo una wasiwasi kwamba mchango binafsi au shughuli ya kujitolea inaweza kuchukuliwa kama mchango wa kibiashara, tafadhali tafuta ushauri kutoka idara ya mahusiano.

# Mawasiliano ya nje na mitandao ya kijamii

### Inabidi sote tutoe mawasiliano kwa namna bora

Kila tunachofanya, kila kitu tunachosema, na kila kitu ambacho wadau wetu wanazungumza kuhusu sisi inaweza kuathiri sifa ya Diageo. Katika dunia iliyounganishwa, ambapo taarifa husafiri duniani haraka sana ndani ya muda mfupi, ni muhimu tusimamie vizuri mawasiliano na wadau wetu wa nje, wakiwemo wawekezaji, vyombo vya habari, wawakilishi wa jamii au serikali, washirika wa biashara, wateja na wanunuzi wa bidhaa zetu.

Mawasiliano ya kila siku ya Diageo na vyombo vya habari, Mashirika Yasiyo ya Serikali na jumuiya yanasimamiwa na timu ya mahusiano kitaifa na kimataifa, ambao piawanapaswa kuidhinisha shughuli ya kuzungumza kwa niaba ya kampuni na mahojiano yoyote kwa vyombo vya habari, ikiwa ni pamoja na taarifa ya biashara kwa niaba ya kampuni au kama inahusisha chapa za Diageo. Mawasiliano na wawekezaji yanasimamiwa na timu ya kimataifa ya wawekezaji. Daima unapaswa kuelekeza maswali yote kwa timu inayohusika.

### Fanya jambo sahihi

Unapaswa:

- **kutotoa taarifa** kwa vyombo vya habari kwa niaba ya Diageo bila kibali kutoka kwa kitengo cha mahusiano ya kampuni, au kwa masuala yanayohusu PR (mahusiano ya umma) ya bidhaa, bila idhini ya msimamizi mkuu wa mawasiliano anayehusika wa timu inayoshughulikia bidhaa
- **kuwasilisha hatua yoyote** ya mwekezaji au mchambuzi wa masuala ya fedha kwa idara ya mahusiano na wawezekaji
- **kuomba kibali** kutoka idara ya mahusiano ya kampuni kabla ya kukubali mwaliko wa kuzungumza au kushiriki katika tukio kwa niaba ya Diageo, Kuwa mwangalifu ili usionekane kana kwamba unaunga mkono watu wa nje, makampuni, bidhaa au huduma bila idhini
- **kuhakikisha matangazo yote ya vyombo vya habari** na taarifa kwa umma zinaidhinishwa kabla ya kuchapishwa na idara ya mahusiano ya kampuni na kwamba mchakato unaofaa wa taarifa umefuatwa
- **kuwa wazi na kusema mambo sahihi** unapotumia mitandao ya kijamii – unapaswa kuwa wazi juu ya uhusiano wako na Diageo na katika mawasiliano binafsi, weka wazi kuwa maoni unayotoa ni yako mwenyewe
- **kufanya maamuzi vizuri** ya mawasiliano katika njia zote za mawasiliano na vyombo vya habari: kamwe usitoe kauli za kupotosha, zenye nia mbaya, zinazokera, zisizofaa, za kibaguzi, vitisho, hasi, zinazokiuka tamaduni za watu, au kauli zisizo na heshima mitandaoni au kwenye majukwaa yoyote ya mawasiliano kuhusu Diageo, wenzako, washindani wetu, au wadau wetu wa nje, washirika wa kibiashara, wateja au watumiaji bidhaa zetu.

# Maswali na Majibu

**Mimi nimekasirishwa na jambo muhimu lililotokea duniani na ninataka kuandika tweet kuhusu suala hilo, lakini naamini baadhi ya watu, wakiwemo baadhi ya wafanyakazi wenzangu, wanaweza kuchukulia maoni yangu vibaya. Ninapaswa kufanya nini?**

Subiri. Fikiria, kama mfanyakazi wa Diageo, ujumbe wako unaweza kuwa na athari hasi kwa sifa ya kampuni, bila kujali kuwa ni maoni yako binafsi. Kwa kawaida pengine ni bora kuacha kutuma ujumbe wa twitter sasa kwa kuandika katika hali hii linaweza lisiwe jambo zuri kwa muda huu.

**Nimepokea mwaliko kuzungumza katika kongamano la tasnia. Nadhani itakuwa ni nafasi nzuri ya kutangaza bidhaa za Diageo. Ningependa kukubali. Je, nahitaji kuongea na mtu yeyote kwanza?**

Ndiyo, unapaswa kujadili mwaliko huo na msimamizi wako na idara ya mahusiano ya kampuni kabla ya kukubali. Kila mara uwe makini kutafuta vibali sahihi wakati unapowakilisha, au kuonekana kuwa msemaji wa, Diageo.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 44**






### Mitandao ya kijamii

Baada ya saa za kazi, iwapo utaamua kuandika ujumbe katika mitandao ya kijamii (yaani, makala ya blogu, ujumbe wa twitter, kutuma ujumbe kwenye mtandao wa kijamii) kuhusu kampuni, bidhaa zetu, sekta ya pombe au suala lingine lolote linalohusiana na Diageo, unapaswa ueleze wazi kwamba maoni unayotoa ni yako mwenyewe na sio ya Diageo. Lazima uchukua muda zaidi wa kufikiria uamuzi kabla ya kutoa maoni yako, na jiulize swali lifuatalo: 'Je, ninachosema kinaweza kuiletea picha mbaya Diageo, bidhaa zetu, au wadau wetu?' Ikiwa jibu ni 'ndiyo' au 'inawezekana,' acha usitume. Kwa msaada zaidi au ushauri, rejelea Miongozo ya Diageo kuhusu Mitandao ya Kijamii kwa Wafanyakazi.

# Mahusiano na wateja, wasambazaji bidhaa na washirika wengine wa biashara

### Tunatarajia washirika wetu wa biashara watatumia kanuni hizi za msingi katika shughuli zao kama ilivyo kwenye kanuni hii

Tunataka kufanya biashara na washirika ambao wanafuatilia maadili yetu. Tunawahimiza washirika wetu wote kupitisha ahadi za wazi kuhusu maadili ya biashara kama zile za Kanuni yetu, na mtu yoyote anayetenda kazi kwa niaba ya Diageo ni lazima ahakikishe kwamba matendo yao yanazingatia Kanuni na sera zetu. Iwapo unawajibikia mahusiano na mshirika wa kibiashara, unapaswa kuhakikisha kwamba mienendo yake inaendana na viwango vyetu.

Tunatarajia pasi na shaka kuwa washirika wetu wa kibiashara:

- watazingatia sheria zote muhimu, masharti, na viwango vya sekta vinavyohusika
- wanafahamu Kanuni zetu za Kufanya Biashara na matarajio yetu na kwamba watazingatia kanuni zetu za Kufanya Biashara katika shughuli zao wenyewe
- kuendesha biashara kwa uadilifu na kwa uaminifu.
- kuheshimu haki za binadamu na viwango vya msingi vya kazi
- wanathamini tofauti na kuonyesha nia ya dhati kujenga mazingira bora ya kazi yanayojali haki na usawa
- kuweka mazingira bora na salama ya kufanyia kazi
- wawe na msimamo thabiti wa mazingira endelevu
- kuwa na msimamo mkali wa kutopokea hongo na rushwa ya aina yoyote ile, ikiwemo kudai malipo kwa nguvu au malipo mengine yasiyofaa kama vile malipo ya kuwezesha shughuli fulani, na kusema wazi kama wana uhusiano wowote na viongozi wa serikali (angalia ufafanuzi kwenye ukurasa wa 17)
- kuepuka na hali ambapo mgongano wa maslahi unaweza kutokea, na wakati wote ueleze kama kuna uwezekano wa mgongano
- kutovumilia ukwepaji wa kulipa kodi au ushuru popote wanapofanya kazi na uwezeshaji wa ukwepaji kulipa kodi na ushuru kwa mtu mwingine
- kuchukua hatua mapema kulinda taarifa za siri na za binafsi na kuheshimu haki za usiri wa data za mtu.

### Fanya jambo sahihi

Diageo inajitolea:

- **kuhakikisha** kila kampuni hata isiyomilikiwa kwa asilimia zote na kampuni tanzu na kila kampuni kwenye ubia inafuata Kanuni za Maadili ya Kibiashara na sera nyingine zinazolingana na misingi yetu
- **kuhamasisha** washirika wetu katika ubia kwamba hatuwalazimishi kutimiza masharti ya Kanuni zetu katika ubia na kwenye shughuli zao wenyewe.

Unapaswa:

- **kuhakikisha** kwamba watu wengine wanaofanya kazi kwa niaba ya Diageo (ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wa muda na wenye mkataba, washauri na mawakala) wanafahamishwa kuhusu Kanuni na matarajio yetu na kwamba wanazitii, wahimize wasambazaji wetu kutumia kanuni zile zile za msingi za Kanuni zetu katika shughuli zao wenyewe, na kuelewa na kutii Kiwango cha Ushirikiano wa Kimataifa na Wasambazaji
- **kufuata masharti** ya Sera ya Kimataifa ya Ununuzi ikiwa unatafuta na kununua bidhaa au huduma kwa niaba ya Diageo
- **kukamilisha** taratibu za Mjue Mteja Wako (KYC) na Mjue Mshiriki wako wa Biashara (KYBP), kama inavyotakiwa, na mshirika wa biaashara.

**Washirika wa kibiashara** *wanaweza kutoa taarifa pia kupitia huduma ya speak up*

Tunatarajia washirika wetu wa biashara kutoa taarifa ya viashiria vinavyoonyesha uwezekano wa ukiukwaji wa Kanuni yetu, na hata ukiukwaji wenyewe kwa mkuu wa mawasiliano Diageo, mwanasheria wa ndani wa Diageo au kwa siri kupitia huduma ya SpeakUp (angalia ukurasa wa 45).

**Tunaangalia kila habari kwa umakini na na hatutakubali ulipizaji kisasi wa aina yoyote na mfanyakazi dhidi ya mshiriki wa biashara aliyetuletea habari au anayetusaidia uchunguzi.**

**Kwa taarifa zaidi kuhusu unachohitaji kusoma, tazama ukurasa wa 44**



# Unachohitaji kusoma

| Mada | Unachohitaji kusoma (Mambo yote haya yanaweza kupatikana kwenye Mosaic) | | | Tunaotarajia wasome haya |
|---|---|---|---|---|
| | Sera | Kiwango | Nyingine | |
| Kunywa kwa uangalifu | Pombe ya Wafanyakazi | | DRINKiQ (DRINKiQ.com) | Wafanyakazi wote<br>Wafanyakazi wote |
| Biashara ya ndani | Kanuni ya Diageo ya Kujihusisha katika Dhamana | | | Kama unaamini una habari ya ndani hasa kama wewe unatarajia kushugulikia hisa za Diageo au dhamana |
| Migongano ya maslahi | Ununuzi wa Zawadi na Burudani | Kupanga<br>Kushirikiana na Wasambazaji | | Wafanyakazi wote<br>Ikiwa unasimamia mahusiano na wauzaji<br>Ikiwa unahusika kwenye mchakato wa manunuzi |
| Masoko na ubunifu | Kanuni ya Masoko ya Diageo (DMC)<br>Kanuni ya Diageo ya Kidijitali | Utafiti Unaofaa<br>Taarifa za Mtumiaji za Diageo Kimataifa | Miongozo ya Lazima ya Mitandao ya Kijamii ya Diageo | Masoko, ubunifu mauzo, mahusiano ya kampuni na sheria<br>Ikiwa unahusika katika kipengele chochote cha masoko ya kidijitali<br>Ikiwa unahusika katika kipengele chochote cha masoko ya kidijitali<br>Ikiwa unahusika katika kipengele chochote cha utafiti wa mtumiaji bidhaa au mteja<br>Ikiwa unahusika kuweka chapa bidhaa zetu |
| Zawadi na burudani | Zawadi na Burudani<br>Kukabiliana na Ufisadi | | Fomu ya Maombi ya Kabla ya Idhini Zawadi, Burudani au Ufadhili<br>kwa Maafisa wa Serikali | Wafanyakazi wote<br>Wafanyakazi wote<br>Wafanyakazi wote |
| Rushwa na ufisadi | Kukabiliana na Ufisadi<br>Zawadi na Burudani | Mjue Mshirika Wako wa Biashara (KYBP) | | Wafanyakazi wote<br>Wafanyakazi wote<br>Ikiwa unahusika katika kuwakaribisha wateja na wauzaji, au ikiwa unafanya kazi kwenye idara ya sheria |
| Serikali na vyama vya kisiasa | Kukabili Ufisadi<br>Zawadi na Burudani | | | Wafanyakazi wote<br>Wafanyakazi wote |
| Biashara haramu | Kukabiliana na Ufisadi | | | Kama upo katika idara ya mauzo, masoko, manunuzi/mabadiliko ya chapa, mahusiano ya kampuni au sheria |
| Mashindano | Ushindani na Sheria ya kudhibiti Ushindani | | Miongozo ya Sheria ya Ushindani ya soko lako<br>Fahamu Miongozo ya Ushindani<br>Zingatia Miongozo yako ya Mawasiliano ya Lugha | Nyaraka hizi nne zinatumika kwa wafanyakazi wote katika idara za mauzo, masoko, fedha, mahusiano ya kampuni na sheria. Pia ni muhimu kwa ugavi na manunuzi, kutegemea jukumu na cheo. |
| Ulaghai | Kukabiliana na Ufisadi | Mjue Mshirika Wako wa Biashara (KYBP) | | Wafanyakazi wote<br>Ikiwa unahusika katika kuwakaribisha wateja na/au wauzaji, au ikiwa unafanya kazi kwenye idara ya sheria |
| Utakatishaji fedha na kusaidia ukwepaji kodi | Kukabiliana na Ufisadi | Mjue Mshirika Wako wa Biashara (KYBP) | | Hati hizi mbili zinatumika kwa wafanyakazi wote wa idara za fedha, mauzo, sheria, ugavi, manunuzi na wafanyakazi wengine wote wanaohusika na kukaribisha wateja na/au wauzaji |
| Vikwazo | Kukabiliana na Ufisadi | Mjue Mshirika Wako wa Biashara (KYBP) | Mwongozo wowote wa eneo husika | Mada hii inahusu wafanyakazi katika idara za fedha, mauzo, sheria, ugavi, manunuzi, biashara, biashara ya fedha, kodi, hazina, Mdhibiti, au anayehusika katika kukaribisha wateja na/au wauzaji au katika kuingiza au kusafirisha bidhaa |
| Afya, ulinzi na usalama binafsi | Usalama wa Afya na Ustawi<br>Usalama wa Kampuni | | Sera ya afya na usalama wa eneo lako na miongozo ya ulinzi<br>Usalama wa Usafiri<br>Miongozo ya Kupanga Hafla na Udhibiti wa Hatari | Wafanyakazi wote<br>Wafanyakazi wote<br>Ikiwa wewe ni kiongozi au unasafiri kikazi<br>Ikiwa unasafiri kikazi au unafanyia kazi mbali na eneo lako la kawaida la Diageo<br>Ikiwa unahusika katika kuandaa au kuendesha tukio |

# Unachohitaji kusoma

| Mada | Unachohitaji kusoma (Mambo yote haya yanaweza kupatikana kwenye Mosaic) | | | Tunaotarajia wasome haya |
|---|---|---|---|---|
| | **Sera** | **Kiwango** | **Nyingine** | |
| Ubaguzi na unyanyasaji | Haki za Binadamu<br>Utu Kazini | | | Wafanyakazi wote<br>Wafanyakazi wote |
| Haki za binadamu | Haki za binadamu | Kushirikiana na Wasambazaji<br>Mtangazaji wa Chapa | | Wafanyakazi wote<br>Ikiwa unafanya kazi na wauzaji |
| Usimamizi wa taarifa na usalama | Usimamizi wa Taarifa na Usalama<br>Matumizi Yanayokubalika | Kushughulikia Taarifa | Miongozo ya Mahali pa Taarifa | Ikiwa unatumia kompyuta ya kawaida, kompyuta mpakato, au simu ya mkononi kufanya kazi<br>Ikiwa unaandika au kushughulikia hati zozote |
| Taarifa za faragha za data na binafsi | Faragha ya Data<br>Kanuni ya Kidijitali ya Diageo<br>Usimamizi wa Taarifa na Usalama | | Taratibu za Diageo za Kushughulikia Migogoro | Wafanyakazi wote<br>Ikiwa unashughulika na taarifa za mtumiaji bidhaa kama sehemu ya shughuli za masoko au ubunifu<br>Ikiwa unashughulika na taarifa binafsi<br>Ikiwa unahusika katika tukio la ukiukwaji wa taarifa binafsi |
| Mali ya kampuni na rasilimali | Usafiri na Gharama<br>Manunuzi | | Sera hizo hizo, viwango na miongozo iliyoandikwa kwa ajili ya usimamizi wa taarifa na sehemu ya usalama | Wafanyakazi wote<br>iwapo unashiriki katika utafutaji na manunuzi ya bidhaa au unatoa huduma kwa niaba ya Diageo; unawajibika na bajeti; unatumia kadi ya manunuzi (P-Card); au iwapo utaandaa ombi la manunuzi |
| Rekodi za biashara | Usafiri na Gharama | Mjue Mshirika Wako wa Biashara (KYBP)<br>Taarifa ya Mamlaka (SoA) | Mazoea ya mwisho ya Kipindi cha Maswali na Majibu | Hususani kama wewe ni kiongozi mwandamizi au unahusika katika miamala mikubwa ya fedha kuliko kawaida kando na shughuli za kila siku za biashara<br>Wafanyakazi wote<br>Ikiwa unahusika kukaribisha wateja na wauzaji, au kama unafanya kazi katika sheria<br>Kama upo katika timu ya biashara au biashara ya fedha kama unahusika na fedha au kuuza bidhaa/huduma kwa niaba ya Diageo |
| Ubora | Ubora | | | Kama unashiriki katika sehemu yoyote ya kutafuta masoko, ubunifu, usambazaji na uuzaji wa bidhaa zetu |
| Uendelevu wa Mwanzo hadi Mwisho | Mazingira | Kushirikiana na Wasambazaji | Miongozo ya Ufungaji Endelevu<br>GREENIQ | Wafanyakazi wote<br>Ikiwa unahusika katika ufungashaji wa bidhaa zetu<br>Ikiwa unafanya kazi na wasambazaji<br>Wafanyakazi wote |
| Michango kwa vyama vya kujitolea | | | Sehemu ya Hongo na rushwa ya Kanuni yetu(ukurasa wa 16/17)<br>Sehemu ya Zawadi na burudani ya Kanuni zetu (pukurasa wa 15) | Wafanyakazi wote<br>Wafanyakazi wote |
| Mawasiliano ya nje na mitandao ya kijamii | Mawasiliano ya Nje<br>Kanuni ya Diageo ya Kidijitali | | Miongozo ya Mitandao ya Kijamii kwa Wafanyakazi | Kama ukijihusisha na vyombo vya habari; kuwasiliana nao kama mwakilishi wa Diageo katika matukio ya umma au makongamano; au wanauliza kuchangia makala, vitabu, utafiti au ridhaa zingine<br>Wafanyakazi wote<br>Iwapo unajishughulisha kwa njia yoyote kuwashirikisha wafanyakazi wetu ili kusaidia kampeni ya masoko ya Diageo('wito wa kuchukua hatua') |
| Mahusiano na wateja, wasambazaji na washirika wengine wa biashara | Manunuzi | Kushirikiana na Wasambazaji<br>Mjue Mshirika Wako wa Biashara (KYBP) | Taratibu za Mjue Mteja Wako (KYC) | Iwapo unafanya kazi na wauzaji<br>Kama unashiriki katika utafutaji na manunuzi ya bidhaa au unatoa huduma kwa niaba ya Diageo; unawajibika katika bajeti; kutumia kadi ya manunuzi (P-Card); au ikiwa unaandaa ombi la manunuzi<br>Ikiwa unahusika katika kuwakaribisha wateja na wauzaji, au ikiwa unafanya kazi kwenye sheria |

# Msaada, ushauri na kueleza wasiwasi...

## Sote tunahitaji mwongozo katika hali fulani - usiogope kuomba msaada

Kila hali ni tofauti, na hakuna kanuni, sera au kiwango kinachoweza kusimamia kila kitu. Ikiwa una wasiwasi wowote kuhusu nini cha kufanya kwa usahihi, unapaswa kuomba msaada au ushauri.

**Toa taarifa kupitia huduma ya Speak Up unapoona ukiukwaji wa maadili au sheria.**

Kama unaamini kuwa kuna kitu kinachofanywa ambacho wewe unaona ni makosa, unapaswa kusema. Sote tunatarajiwa kutoa taarifa haraka kuhusu ukiukaji wa aina yoyote wa Kanuni yetu, sera au viwango. Masuala mengine ambayo lazima yaripotiwe ni pamoja na taarifa au tuhuma kuhusu ukiukwaji wa sheria, wa uhasibu, au matakwa ya kiudhibiti, au mwenendo wowote wenye kutia shaka.

## Kutovumilia kabisa ulipizaji kisasi

Kutoa malalamiko au kuongea kuhusu jambo kunahitaji ujasiri, na wakati mwingine kinachotufanya tusiseme ni hofu ya kusemwa na wenzako au wasimamizi wako.

Tafadhali tunakuhakikishia kuwa Diageo haitavumilia ulipizaji kisasi wa aina yoyote dhidi ya mtu yeyote atakayeripoti tatizo au kusaidia uchunguzi.

## Nitamwambia nani:

Ikiwa unatafuta ushauri au kutoa hisia zako unapaswa kwenda kwa msimamizi wako au, ukiweza, msimamizi yeyote wa ngazi za juu. Wafuatao pia wanaweza kukusaidia:

Kiongozi wa maadili katika biashara yako ya ndani

Mwanasheria wa ndani wa Diageo

Idara ya Rasilimali Watu

Timu ya maadili ya kazi Duniani
business.integrity@diageo.com

### Huduma yetu ya siri ya SpeakUp

Kama unaamini Kanuni, sera au viwango vyetu vimekiukwa, na hutaki kuzungumza na mtu aliye ndani ya kampuni, unaweza kutumia SpeakUp ili kutoa malalamiko yako.

Hii ni huduma ya siri kwa ajili ya kutoa mashtaka kuhusu mwenendo wa biashara au masuala ya uzingatiaji na maadili.

## SpeakUp

SpeakUp inasimamiwa na kampuni nje ya Diageo, na inafikiwa na watu ambao wanazungumza lugha nyingi. Kama utawasiliana na SpeakUp, watakuuliza jina lako, lakini hawatasema kama hupendi kufanya hivyo, na watalinda maelezo yako kwa siri, isipokuwa kama haja ya kusema kwa mujibu wa mchakato wa kisheria au uchunguzi wa serikali. Unaweza, kama sheria inaruhusu, kutotajwa jina, na hakuna mtu atakayejaribu kujua wewe ni nani. Lakini, ukiwapa jina lako utaweza kusaidia uchunguzi katika suala ulilolibua, kwa sababu inatuwezesha kuwasiliana na wewe iwapo tuna maswali au kuhitaji maelezo zaidi.

**Unaweza kupata maelezo zaidi ya mawasiliano ya SpeakUp kwenye MOSAIC na katika www.diageospeakup.com**

Toleo la Agosti 2023

Diageo plc
16 Great Marlborough St,
London W1F 7HS
Uingereza
Simu +44 (0) 20 8978 6000
www.diageo.com

Imesajiliwa Uingereza
Nambari 233078

Kanuni hii inapatikana katika Mosaic, na katika www.diageo.com katika lugha zifuatazo:

Kiamhari
Kibahasa cha Indonesia
Kichina (kilichorahisishwa)
Kichina (cha kawaida)
Kidachi
Kifaransa
Kijerumani
Kigiriki
Kitaliano
Kijapani
Kikorea
Kipoli
Kireno
Kirusi
Kihispania
Kiswahili
Kitai
Kituruki
Kivietnam

DRINKiQ.com
Drink Responsibly. drinkaware.co.uk
for the facts